# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 1, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581877

www.ippmedia.com

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com

MIAKA 30 Nipashe


UKURASA WA 2

**Ruto** apokea kijiti uenyekiti wa EAC, ataja vipaumbele sita



UKURASA WA 5

**Gharama** matibabu kwa magonjwa yasiyoambukiza sasa pasua kichwa



UKURASA WA 11

MAISHA YALIVYO

**Kupuuzia** ndoto za usiku kunavyotesa watu wengi

## RIPOTI MAALUM

# Tahadhari wanaokatisha hedhi kwa kutumia dawa

• **Wako** hatarini kupata saratani na utasa, wenyewe watoa sababu... *Endelea ukurasa 4*





UKURASA WA 22

## ARSENAL KUTOSAJILI JANUARI

ARSENAL itatafuta kuimarisha kikosi cha Mikel Arteta mnamo 2025 lakini hakuna uwezekano...

## CHAUMMA wala ubwabwa kisa ushindi kiti kimoja uenyekiti wa mtaa

UKURASA 2



## Manusura jengo Kariakoo asimulia masahibu aliyopata

UKURASA 3

MICHEZO YANGA SC, SIMBA ZAKWEPANA ALGERIA UK.24 KATUNI UK.6

# Ruto apokea kijiti uenyekiti EAC, ataja vipaumbele sita

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAKUU wa Nchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wamemwidhinisha Rais William Ruto wa nchini Kenya kuwa Mwenyekiti Mpya wa jumuiya hiyo, baada ya Rais Salva Kiir wa Sudan Kusini, kumaliza muda wake.

Akizungumza baada ya kushika kijiti hicho, Rais Ruto alitaja vipaumbele sita atakavyovisimamia kipindi chake cha uongozi ikiwamo kuboresha maisha ya watu wa EAC.

Ruto alisema atahakikisha anaongeza ushindani wa kibiashara, kukuza uzalishaji na uongezaji thamani wa bidhaa za ndani ya jumuiya hiyo.

Kipaumbele kingine alikitaja ni kuongeza imani miongoni mwa nchi wanachama na kuimarisha uwekezaji kwa faida ya uchumi EAC.

"Hivi ndivyo vipaumbele vyangu vya muhimu kwa ajili ya kuleta mageuzi ya uchumi wa EAC, kutengeneza ajira na kuhakikisha kuna maendeleo endelevu kwa nchini zote, amani, usalama na utulivu,"alisema.

Alisisitiza pia kusimamia suala la uwajibikaji wa kisiasa na utawala bora kwa kuwa ndiyo njia bora ya kuhakikisha uwapo wa utulivu endelevu katika jumuiya hiyo.

Alisema ili kufikia hayo, ni lazima EAC kuendelea kuimarisha mifumo ya kikanda ambayo inalinda mamlaka yao na usalama wa pamoja, huku akihimiza utawala jumuishi unaoakisi matarajio ya wananchi wa Afrika Mashariki.

"EAC ni Jumuiya yenye soko kubwa kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu zaidi ya milioni 300 linalotoa fursa ya kujenga uchumi na kuimarisha biashara kwa manufaa ya watu wa EAC,"alisema.

Kuhusu lugha za Kiswahili, Kiingereza na Kifaransa, Rais Ruto alisema zitaendelea kutumika katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, huku akisisitiza Kiswahili kubeba utamaduni wa watu wa Afrika na EAC.

Alimshukuru aliyempokea nafasi hiyo, Rais Kiir kwa uongozi wake wenye maono ulioiletea EAC mafanikio makubwa.

Awali, Rais Kiir kabla hajakabidhi uongozi kwa Rais Ruto, alisema suala la amani na usalama linapaswa kupewa kipaumbele .

Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa Mkutano wa 24 wa kawaida wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya hiyo uliofanyika jijini hapa, aliwataka wananchi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kujivunia Jumuiya hiyo kwa kuwa kuna mwanga mkubwa wa matumaini mbeleni.

Rais Samia aliwahakikishia wananchi wa EAC kuwa changomoto zozote zitakazoibuka hazitapewa nafasi ya kuwavunja moyo na kuwarudisha nyuma.

Alisema changamoto zinapoibuka baadhi ya watu hudhani ndiyo mwanzo wa jumuiya hiyo kusambaratika.

"Tunataka kuhakikishia watu wote tunakuwa wamoja na jumuiya moja, hivyo tunaposherehekea miaka 25, EAC inazidi kuimarika na kuelekea katika utangamano zaidi kama wimbo wetu wa EAC unavyosema, Kwa hiyo wananchi tujivunie jumuiya yetu," alisema.

Rais Samia alipongeza mafanikio yaliyofikiwa na EAC kwa miaka 25 ikiwamo kuongezeka kwa idadi ya wanachama kutoka watatu mwaka 1999 hadi kufikia wanane sasa.

"Lakini ninakupongeza Rais Ruto kwa kuchukua nafasi ya Uenyekiti wa EAC na Rais Kiir aliyemaliza muda wake," alisema.

Katibu Mkuu wa EAC, Veronica Nduva alisoma takribani maazimio saba ya Wakuu wa Nchi za EAC ikiwamo kukiidhinisha Kiswahili kuwa moja ya Lugha rasmi za EAC baada ya Kiingereza na Kifaransa.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz***

# CHAUMMA wala ubwabwa kwa ushindi kiti kimoja uenyekiti mtaa

**Na Grace Mwakalinga**

CHAMA cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA), kimefanya sherehe kwa kupika ubwawa baada ya mgombea wake, Brian Mwakalukwa, aliyekuwa akigombea nafasi ya uenyekiti wa Mtaa wa Soko, Halmashauri ya Jiji la Mbeya kuibuka mshindi.

Sherehe hiyo ilifanyika jana eneo la Soko la Mwanjelwa ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa sera ya chama hicho chini ya mwenyekiti wake, Hashim Rungwe, inayosema 'Kupeleka ubwabwa shuleni na hospitalini'.

Mwenyekiti wa CHAUMMA Mkoa wa Mbeya, Ipyana Samson, alisema jana kuwa katika Mkoa wa Mbeya walisimamisha wagombea 130 kwa nafasi Uenyekiti wa Serikali za Mitaa, Vitongoji, Vijiji na wajumbe wa nafasi mchanganyiko na kundi la wanawake.

Alisema kati ya wagombea wote, Mwakalukwa ndiye aliyeibuka mshindi baada ya kuchaguliwa na wananchi kwa kura 42 akifuatiwa na mgombea wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) aliyepata kura 38.

"Ni ushindi pekee wa chama chetu si tu kwa Mkoa wa Mbeya, bali nchi nzima. Hii ni ishara kuwa tunaaminiwa na wananchi kuibuka kidedea hasa katika eneo hili la mjini, tunajipanga kwa Uchaguzi Mkuu hapo mwakani tutaongeza wanachama kutoka 300 wa sasa vilevile tutashimamisha wagombea kwenye nafasi za udiwani na ubunge," alisema Samson.

Alisema sherehe hiyo ya ubwawa imefanikishwa na wafanyabiashara wa Soko Kuu la Mwanjelwa, eneo ambalo mgombea wao ameshinda ambapo wametoa fedha kwa ajili ya kununua mchele na mahitaji mengine.

Aliyekuwa mgombea wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Ive Alex, alisema amefurahia mchakato wa uchaguzi ulivyokwenda hadi mgombea wa CHAUMMA kuibuka kidedea.

Alisema Mwakalukwa ni kiongozi aliyejaliwa hekima na busara na anatimiza majukumu yake kulingana na mahitaji ya wafanyabiashara.

Atupokile Eliachim, mkazi wa Mtaa wa Soko, mshindi wa nafasi ujumbe kwa tiketi ya CCM, alisema amefurahishwa na ushindi wa Mwakalukwa na kuahidi kumpa ushirikiano mwenyekiti huyo, katika kutimiza majukumu yake.

Mwakalukwa alisema uchaguzi huo ulikuwa huru na haki na kuwaahidi wananchi kusimamia masuala ya usafi na uzoaji taka kuzunguka maeneo yote sokoni hapo ambapo ni moja ya changamoto kubwa. Rungwe alijizolea umaarufu katika kampeni ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ambapo alijinadi na sera ya ubwabwa, ambayo ilizua gumzo.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz***



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Rais wa Sudan Kusini, Salva Kiir, katika mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kabla ya kuanza kwa Mkutano wa kawaida wa 24 wa viongozi hao pamoja na maadhimisho ya miaka 25 ya Jumuiya hiyo katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC) Jijini Arusha jana. **PICHA: IKULU**

# Masauni asisitiza nyumba za ibada kuhamasisha amani

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni amesisitiza Watanzania kuendelea kudumisha amani sambamba na kutumia nyumba za ibada kuhamasisha na kutoa mafundisho ya dini yatakayodumisha amani.

Waziri Masauni aliyasema hayo juzi wakati akifungua Msikiti wa Tawhid eneo la Coco Beach (Zamani Msikiti wa Makuti).

"Tanzania ni nchi ambayo tunavumiliana sana na ndio maana ni rahisi kukuta watu wenye dini tofauti wanaishi kwa upendo, mshikamano bila kubaguana wala kuchukiana," alisema.

Masauni alisema utamaduni wa kuvumiliana umejengewa misingi imara na waasisi wa taifa.

Alisema ndio maana dini moja huweza kusaidia mchango wa ujenzi nyingine na suala hilo limezidisha amani nchini.

Mwenyekiti wa Taasisi ya The Islamic Foundation, Aref Nahd, alisema kukamilika kwa msikiti huo kutasaidia waumini kutekeleza ibada ya swala tano kwa waislam wanaokwenda katika fukwe hizo kutembea na kupumzika.

Ufunguzi huo pia, ulihudhuriwa na Balozi wa Qatar nchini, Fahad Rashid Al Marekhi, Balozi wa Uturuki nchini, Dk. Mehment Gulluoglu, mashehe na waumini wa dini hiyo.

# Biashara China, Tanzania yafikia dola bilioni nane

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema uhusiano wa kibiashara kati ya Tanzania na China umeendelea kukua ambapo mwaka 2023 biashara kati ya nchi hizo ilifikia Dola za Kimarekani bilioni 8.78.

Amesema kuwa ukuaji na ushirikiano huo wa kampuni za China na wafanyabiashara wa Tanzania umeleta maendeleo katika ukuaji wa viwanda vya ndani, kutengeneza ajira, ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa hali ya maisha ya Watanzania.

Majaliwa aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya Kumbukumbu ya 10 ya Jumuiya ya Kukuza Ushirikiano kati ya China na Tanzania, iliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Chuo Kikuu cha Dar ea Salaam (UDSM).

Alisema kampuni za China zimezindua takribani miradi 1,274 ambayo kwa kiasi kikubwa pamoja na mambo mengine, imezalisha ajira kwa Watanzania.

"Huu ni uthibitisho wa namna ushirikiano wetu unavyolenga kutoa fursa kwa wananchi wetu" Rais Samia Suluhu Hassan anathamini mchango wa China katika maendeleo ya Tanzania katika sekta mbalimbali zikiwamo za biashara, miundombinu na utamaduni," alisema.

Majaliwa alisema China ni moja ya mshirika mkubwa wa kibiashara na uwekezaji kwa Tanzania na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika maendeleo katika sekta za kilimo, madini, viwanda na maendeleo ya miundombinu.

Alisema China imekuwa mshirika muhimu katika kuisaidia Tanzania kukabiliana na majanga ya kiafya ikiwamo magonjwa ya kuambukiza na changamoto za afya ya mama na mtoto.

"China imekuwa ikitoa timu za wataalam, kuchangia vifaa, na kusaidia kujenga miundombinu ya afya. Ushirikiano huu umeokoa maisha ya wengi na umehakikisha kwamba watu wetu wanapata huduma bora za matibabu," alisema.

Akizungumza kuhusu Jumuiya ya Kukuza Urafiki kati ya Tanzania na China, Majaliwa alisema jumuiya hiyo imekuwa mchango mkubwa katika kukuza na kuendeleza uhusiano kati ya mataifa hayo mawili ikiwamo kimeleta watu pamoja, si tu kutoka kwa serikali, bali kutoka nyanja mbalimbali za maisha.

Naibu Waziri wa Wizara Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Cosato Chumi, akizungumza kwa niaba ya Waziri wake, alisema jumuiya hiyo imeendelea kutumika kama msingi wa kukuza maelewano na ushirikiano kupitia sekta za elimu, afya, utamaduni na biashara

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo na Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda, alisema jumuiya hiyo ni matunda ya uhusiano mzuri uliopo kati ya Tanzania na China ambayo kwa kipindi kirefu yamechangia kwa kiasi kikubwa kukuza na kuwezesha maendeleo nchini katika sekta mbalimbali ikiwamo miundombinu, kilimo, biashara na afya.

# Manusura jengo Kariakoo asimulia yaliyomkuta

**Na Restuta James**

MANUSURA wa jengo lililoporomoka la biashara Kariakoo, Dar es Salaam na kusababisha vifo vya watu 31 na wengine 88 kujeruhiwa, Kunti Abdallah, amesimulia masahibu yaliyomkuta.

Amesema wakati likiporomoka, alikuwa ndani ya jengo hilo na alianza kufanya maombi akiwa katikati ya vifusi hivyo na kumwezesha kutoka salama.

Mfanyabiashara huyo ambaye ni miongoni waliookolewa baada ya jengo hilo kuporomoka Novemba 16, mwaka huu, ametoa ushuhuda huo juzi katika mkesha wa maombi uliofanyika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Kinondoni, Dar es Salaam.

Akishuhudia waumini wenzake, Kunti alisema alikuwa sakafu ya kwanza kati ya tatu zilizokuwa katika jengo hilo.

Alisema akiwa amefunikwa na kifusi, katika hali ya kushangaa, alikumbuka kumwita Yesu, kisha alipata amani kwamba atatoka salama.

"Niliita Yesu mara tatu, nikaanza kusikia maporomoko ya kifusi yakianguka juu ya mwili wangu. Nikasikia uzito na kila kitu kikanielemea.

"Sakafu zote za mizigo zilizokuwa juu yetu, zilituporomokea," alishuhudia Kunti huku akibubujikwa na machozi.

Alisema aliendelea kuomba akiwa ndani ya kifusi ilhali amebanwa mwili mzima na baada ya muda, alipata ujasiri wa kufungua macho na kuona nafasi ndogo iliyojitengeneza na kusaidia kumwingizia hewa.

"Nilianza kupata hewa. Nikaanza kumshukuru Mungu na kuimba nikiomba Yesu asinipite. Namshukuru Mungu, walikuja vijana wabeba mizigo ambao waliniambia, walikuta mguu wangu unacheza na walisikia sauti kwa mbali nikiimba.

"Kama si kumwita Yesu, nisingepona. Mimi nilikuwa mwisho kabisa wa jengo," alisema Kunti aliyeokoka miaka mitatu iliyopita baada ya kubatizwa katika Usharika wa Keko, mkoani humo.

Kunti ni mmoja wa manusura wa ajali ya kuporomoka kwa jengo la ghorofa tatu lililokuwa mitaa ya Mchikichi na Congo, Kata ya Kariakoo, iliyotokea siku hiyo saa 3:00 asubuhi na kusababisha vifo vya watu 31 na kujeruhi 88.

Tayari wamiliki wa jengo hilo wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu na kusomewa mashtaka 31 ya kuua bila kukusudia.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @guardian.co.tz*

# Mpango: Dk. Ndugulile alikuwa mtetezi wa maslahi ya taifa, kiongozi mwenye nidhamu

**Na Romana Mallya**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiifariji familia ya aliyekuwa Mbunge wa Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (W H O), Kanda ya Afrika marehemu, Dk. Faustine Ndugulile, wakati alipowasili nyumbani kwa marehemu Kigamboni Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU YA RAIS**

MAKAMU wa Rais wa Dk. Philip Mpango, amesema marehemu Dk. Faustine Ndugulile, Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika, alikuwa kiongozi mwenye nidhamu, rafiki wa kila mtu na kiongozi aliyetetea vyema maslahi ya taifa.

Dk. Ndugulile ambaye ni Mbunge wa Kigamboni, Dar es Salaam, alifariki dunia Jumatano ya wiki hii wakati akiendelea na matibabu nchini India kwa maradhi yaliyokuwa yanamkabili na mwili wake kuwasili Tanzania juzi.

Akizungumza nyumbani kwa marehemu Kigamboni alikoenda kwa ajili ya kuifariji familia yake, Dk. Mpango amewaombea faraja na moyo wa uvumilivu walioguswa na msiba huo.

Aliwashukuru wote walioshiriki katika kuifariji familia hiyo katika kipindi kigumu kwao na kutoa wito kwa Watanzania kuendelea kushirikiana katika nyakati mbalimbali zinazojitokeza katika jamii ikiwamo za majonzi na furaha.

Dk. Mpango alisema inapaswa kuendelea kumshukuru Mungu kwa maisha ya Dk. Ndugulile hapa duniani.

"Ni vema kwa Watanzania kuendelea kuishi vizuri na ndugu na majirani," alisema. Akiwa nyumbani hapo, Makamu wa Rais amesali pamoja na familia, ndugu, jamaa na marafiki kumuombea marehemu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Ofisi ya Bunge, kesho mwili utatolewa Lugalo na kupelekwa Parokia ya Mtakatifu Immaculata, Upanga, Dar es Salaam, kwa ajili ya ibada na kisha utapelekwa viwanja vya Karimjee kwa ajili ya mazishi ya kitaifa, yatakayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan. Baada ya Karimjee, mwili utalala nyumbani kwake Kigamboni na Jumanne, utapelekwa viwanja vya Machava, Kigamboni kwa ajili ya wananchi wake kumuaga na baadaye utazikwa katika makaburi ya Mwongozo, yaliyoko Kata ya Mwongozo, wilayani Kigamboni.

Dk. Ndugulile aliyezaliwa Machi 31, 1969, alifariki dunia Novemba 27, mwaka huu, akiwa nchini India alikokwenda kutibiwa.

Juzi, Dk. Mpango alifika pia, nyumbani kwa aliyewahi kuwa Msajili wa Hazina Marehemu Dk. Oswald Mashindano, aliyefariki dunia Jumatano ya wiki hii na kuifariji familia yake.

Akizungumza na waombolezaji, Makamu wa Rais aliyeambatana na mwenza wake, Mama Mbonimpaye Mpango, alisema marehemu Dk. Mashindano aliyezikwa jana makaburi ya Kinondoni, amefanya kazi vizuri na kwa uaminifu mkubwa enzi za uhai wake.

Alisema katika nafasi mbalimbali alizowahi kutumikia ikiwamo Msajili wa Hazina aliweza kutoa mchango mkubwa katika taifa kupitia utafiti mbalimbali alizowahi kufanya hususani za maendeleo ya kilimo.

# Hatari wanaokatisha hedhi kwa kutumia dawa

**Na Jenifer Gilla**



NI bomu jipya kwa maisha ya watu. Hivi ndivyo inavyoweza kuelezwa kutokana na hatari inayoinyemelea jamii kutokana na matumizi ya dawa kwa wanawake hasa wakati wa hedhi.

Matumizi ya dawa za kukata hedhi yameshika kasi mijini hali iliyoamsha wataalamu wa afya na kuonya kwamba zinaweza kusababisha saratani, utasa na kuharibu figo.

Wauzaji katika maduka ya dawa waliozungumza na mwandishi wa habari hii, wametaja wanunuzi ni wenye umri kati ya miaka 17 hadi 35.

Uchunguzi uliofanywa na mwandishi wa habari hii mkoani Dar es Salaam umebaini kuwa watumiaji wakuu wa dawa hizo ni wanafunzi wa vyuo, wasafiri na kinadada wanaofanya biashara ya kuuza miili yao.

Mfanyakazi wa maduka ya dawa yaliyoko Ubungo, Dar es Salaam, Happy Kasimu, anasema wengi wanaokwenda kununua dawa hizo ni wasichana walio na umri kati ya miaka 17 na 35 hasa wanafunzi wa vyuo na wale wanaofanya biashara ya kuuza miili.

Anasema kwa kuwa duka lake liko karibu na kumbi za starehe ambazo zina wasichana wengi wanaofanya biashara ya ngono, kwa siku huuza dawa hizo kwa watu watatu hadi wanne na wengine anaowafahamu huwatuma bodaboda.

Wakati uuzaji huo wa dawa holela ukifanyika, Novemba, 2023 Waziri wa Afya (wakati huo), Ummy Mwalimu, alitoa onyo kali kwa wafamasia na wamiliki wa maduka ya dawa wanaotoa dawa bila kuangalia cheti cha daktari.

Akifunga Kongamano la Tatu la Usugu wa Vimelea dhidi ya Dawa na kufungua rasmi Wiki ya Uhamasishaji na Uelimishaji Jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa iliyoanza Novemba 18 hadi 24, mwaka jana, Ummy alisema kufanya hivyo ni kuendeleza tatizo la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa na kuhatarisha afya za watu.

### SIMULIZI WATUMIAJI

Doroth Paula, anasema huwa anakunywa vidonge vya kuzuia hedhi pindi anapokuwa safarini kutoka mkoa mmoja kwenda mwingine.

Anasema hufanya hivyo ili kuepuka usumbufu barabarani wa kutafuta sehemu ya kujisitiri au wakati mwingine kuhofia kuchafuka.

“Usumbufu mwingine ni kupata maumivu makali ya tumbo. Safari ndefu halafu njia nzima unaumwa tumbo hata raha ya safari huioni. Unakosa hamu ya kula na matokeo yake ukifika mwisho wa safari unakuwa mgonjwa zaidi. Ndiyo maana natumia dawa ili kuepuka hayo,” anasema.

Moja ya wanaofanya biashara ya kuuza mwili, Rachel James, mwenye miaka 18 (si jina lake halisi), anakiri kutumia dawa aina ya (anaitaja) kukata hedhi endapo anakwenda kukutana na mtu wake anayemwita wa muhimu hasa wale wanaotoa fedha nyingi.

“Mimi siwezi kuacha fedha bora niende duka la dawa nikanunue dawa nikate ili damu ikate niingize mpunga (fedha) na mambo mengine baadaye,” anasema.

Alipoulizwa kuhusu madhara ya dawa hizo, anasema hafahamu kama kuna madhara bali anachojua ni dawa kama dawa zingine.

“Nikiwa katika hedhi biashara yangu ya kuuza mwili, ninapojua ninakutana na mteja wangu wa mara kwa mara huwa nakunywa dawa ili kukata hedhi,” anasema rafiki yake Rachel aliyejitambulisha kwa jina moja la Angel, mwenye miaka 24.

### WATAALAM WAONYA

Daktari wa Idara ya Magonjwa ya Wanawake na Uzazi Hospitali ya Aga Khan, Dk. Brenda Ovin, anasema kumeza dawa za kuzuia hedhi (progesterone only pill) au dawa za homoni zinazotumika kuchelewesha au kusimamisha hedhi (norethisterone), huathiri mwili wa mwanamke kwa namna tofauti.

Anasema madhara yanategemea aina ya dawa, muda wa matumizi na hali ya kiafya ya mwanamke, ikiwamo mabadiliko ya mzunguko wa hedhi.

“Dawa zinaweza kubadilisha ratiba ya hedhi, kuifanya ichelewe au isiwe na mtiririko wa kawaida baada ya kusimamisha matumizi,” anasema.

Pia anasema inaweza kusababisha mtumiaji kutokwa na damu isiyo ya kawaida na kwamba baadhi ya wanawake hupata matone ya damu yasiyotarajiwa hata baada ya kutumia dawa hizo na wengine kupata maumivu ya kichwa.

“Kuhisi kichefuchefu au tumbo kujaa ni athari nyingine. Dawa hizi zinaweza kusababisha kichefuchefu kwa baadhi ya watumiaji na kuumwa matiti. Dawa za homoni zinaweza kusababisha matiti kuhisi maumivu au kuvimba kwa muda,” anasema Dk. Ovin.

Anatahadharisha kwamba dawa hizo zinapaswa kutumika tu baada ya kushauriana na daktari ili kuhakikisha zinalingana na hali ya kiafya ya mtumiaji.

Dk. Ovin anasema wanawake wenye matatizo ya kiafya kama shinikizo la damu, kisukari au historia ya saratani ya matiti, wanapaswa kuwa waangalifu zaidi.

“Kama ni muhimu kusimamisha hedhi kwa sababu za kiutendaji, kama safari au hafla, ni bora kutumia dawa hizi mara chache tu na si kwa muda mrefu ili kupunguza madhara yake” anashauri.

Daktari mwingine kutoka Hospitali ya Regency, Dar es Salaam, Geoffrey Stanslaus, anasema kama mtumiaji wa dawa za kuzuia hedhi atatumia kwa muda mrefu, anaweza kuathiri ukuta ambao unatoa damu wakati mwanamke anapokuwa katika hedhi.

Pia anasema inaweza kuvuruga mzunguko wa homoni, jambo litakalosababisha kuona mzunguko wa hedhi katika siku tofauti.

Dk. Stanslaus anasema wale wanaofanya tabia hiyo, ukubwani wanaweza kupata saratani inayoanzia katika ukuta wa uzazi. Anasema mfumo wa homoni ukishavurugika unaweza kumsababishia kuongezeka siku za hedhi na kujiweka katika hatari ya kutoshika mimba.

Kuhusu matatizo mengine nje na hayo, anasema jambo hilo ni jipya bado halijafanyiwa utafiti ili kubaini madhara mengine makubwa zaidi ya hayo.

Mtaalam huyo anasema wako wagonjwa wanaokwenda kupatiwa matibabu hospitalini hapo, ambapo sio rahisi moja kwa moja kutambua kwamba sababu ni matumizi ya dawa hizo mpaka mgonjwa mwenyewe asimulie.

Dk. Stanslaus anasema katika uchunguzi wake, wengi wanaofanya hivyo huwa wanakuwa na dharura kama mitihani, harusi na wengine huwa ni tabia za kihuni ili akutane na mtu wake.

Daktari kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja, Nashie Shongopa, anasema tabia ya kunywa dawa za kusitisha hedhi zinasababisha msongo wa mawazo kwa mhusika baadaye.

“Kama hajapima kujua homoni zake zipoje halafu anakunywa dawa hizo ambazo zinaongeza homoni, itamuwiya vigumu kupata ujauzito baadaye na hiyo itamfanya kuwa na msongo wa mawazo,” anasema.

Mtaalam huyo anasema matumizi holela ya dawa bila kufuata ushauri wa mtaalam humweka mtu katika hatari ya kupata tatizo la figo.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Waziri wa Afya, Jenista Mhagama **PICHA:MTANDAO**

## HABARI KITAIFA




Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omari Ubuguyu, akimkabidhi cheti Mwandishi Mwandamizi wa gazeti la Nipashe, Romana Mallya, baada ya Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA) kutambua mchango wake katika kuelimisha umma kuhusu magonjwa yasiyoambukiza jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Gharama matibabu magonjwa yasiyoambukiza pasua kichwa

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema Chama cha Magonjwa Yasiyoambukiza Tanzania (TANCDA) katika kipindi cha miaka 10 kimeongeza uelewa kwa jamii kuhusu magonjwa yasiyoambukiza, ingawa changamoto iliyopo ni gharama kubwa ya matibabu kwa magonjwa hayo.

Mkurugenzi Msaidizi wa Magonjwa Yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Dk. Omari Ubuguyu, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam katika maadhimisho ya miaka 10 ya TANCDA tangu kuanzishwa kwake.

Maadhimisho hayo yalianza na matembezi kutoka ufukwe wa Coco Beach kupita Daraja la Tanzanite hadi mzunguko wa Agha Khan na kisha kurejea Coco Beach.

Katika sherehe hizo, makundi mbalimbali yalitambuliwa kwa kupewa vyeti kutokana na mchango wao, akiwamo Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Romana Mallya. Dk. Ubuguyu alisema miaka mitano ndani ya miaka 10 ya uwapo wa TANCDA, imeongeza uelewa kwa wananchi na kutambua umuhimu wa kupambana na magonjwa yasiyoambukiza ikiwamo kufanya mazoezi.

"TANCDA imeshirikiana na Wizara ya Afya, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutoa mafunzo kwa watoa huduma.

"Miaka miwili iliyopita tumetoa mafunzo kwa watoa huduma takribani 3,000 katika hospitali 710 hasa vituo vya afya nchi nzima ili kuhakikisha huduma inatolewa. Tuliandaa mkakati wa pamoja na TANCDA ikatusaidia kutafuta wadau ili kufanikisha hilo," alisema.

Kadhalika alisema wametengeza mpango wa pamoja wa utafiti wa magonjwa yasiyoambukiza kwa kushirikiana na pia na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na nyingine zinazofanya kazi katika eneo hilo.

Alisema kuna utafiti zaidi ya tano ambazo TNCDA wameshiriki moja kwa moja au kwa kutafuta wafadhili.

"Kuna utafiti ambao unafanyika sasa ambao matokeo bado hatujatoa naomba nisiuzungumzie. Katika utafiti mkubwa wa kitaifa kwa ajili ya kutafuta viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza nchini.

"Tumeshirikiana nao na Shirika la Afya Duniani (WHO) walikuwa wafadhili wa juu lakini baadhi ya maeneo machache TNCDA wameshiriki" alisema.

Dk. Ubuguyu alisema wanafanya utafiti nao wa kuunganisha mifumo ya utoaji huduma za afya hasa katika magonjwa yasiyoambukiza na za moja kwa moja za kuangalia matokeo ya matibabu hasa ugonjwa wa kisukari aina ya kwanza na kinachopata watu wazima.

Kadhalika alisema utafiti za sasa za saratani ambazo zimepata ufadhili kutoka katika chama hicho na zinazolenga jamii kuona vitu gani vipimwe.

Alisema kwa kiwango kikubwa wamesogea katika kufikia Malengo ya Milenia kwa sababu hakuna hata eneo moja ambalo hawajafanyia kazi na kupiga hatua kwa kiwango kikubwa.

Alisema ndani ya miaka 10 changamoto kubwa ni gharama za matibabu hasa wanaougua ambapo hatua zilizochukuliwa na serikali ni kuhakikisha kila Mtanzania anakuwa na Bima ya Afya kwa Wote.

"Kwa hiyo tunatumia mikakati zaidi ya mmoja, kutenga bajeti maalum ambapo serikali inafanya, pili ni mfuko wa pamoja ya bima na wafadhili. TANCDA wamesaidia katika eneo la kuongea na wafadhili, wafadhili wengi hawaipi fedha serikali moja kwa moja huwapa wadau wengine," alisema.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations @ guardian.co.tz***




# Ripoti ya waangalizi uchaguzi wa serikali za Mitaa kutolewa kesho

**Na Waandishi Wetu**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, amesema waangalizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Vijiji, Vitongoji, wanakamilisha ripoti yao ambayo inatarajiwa kutolewa kesho.

Dk. Henga aliyasema hayo juzi alipohojiwa na Nipashe kuhusu maoni yao baada ya matokeo ya uchaguzi huo uliofanyika Novemba 27, mwaka huu kutangazwa.

"Waangalizi wa uchaguzi wanakamilisha ripoti tutaitoa Jumatatu," alisema mkurugenzi huyo wa LHRC.

Mchambuzi wa masuala ya siasa na Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) alisema, "Matokeo ya uchaguzi huu wa serikali za mitaa hayana tofauti na yale ya mwaka 2019, kwani CCM bado imeonekana imeshinda kwa zaidi ya asilimia 90."

Alisema ili kuimarisha demokrasia nchini wanahitaji kuongeza jitihada katika kuimarishwa vyama vya upinzani ili kuleta ushindani.

Dk. Mustapha alisema matokeo yaliyotangazwa yanaonesha kwa namna gani ambavyo vyama vya upinzani havikujipanga ipasavyo kwa ajili ya kushinda.

"Mtazamo wangu ninaona mchakato wa uchaguzi ulikwenda sawa licha ya uwapo wa changamoto ambazo zilikuwa zikilalamikiwa na baadhi ya vyama vya upinzani hasa chama kikuu cha upinzani CHADEMA," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi, Jaji Mstaafu Mbarouk Salimu ametoa onyo kwa wananchi kwa kutojiandikisha kupiga kura au kupiga kura mara mbili.

Alisema kufanya hivyo ni kosa linaloweza mtu kufungwa jela miezi isiyopungua sita au kulipa faini Sh. 100,000 au vyote kwa pamoja.

Akizungumza juzi Mjini Moshi, mkoani Jaji Mbarouk wakati akifungua mkutano wa tume na wadau wa uchaguzi kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapigakura, aliwataka wadau kuendelea kutoa elimu kwa wananchi umuhimu wa kujiandikisha.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Katiba, Dk. Ananilea Nkya, katika maoni yake, alisema ili Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) iwe huru, inatakiwa bajeti yake itengwe kutoka Hazina, badala ya kupitishwa wizarani.

Alisema ipewe nguvu ya kuajiri watumishi wake kwa uhuru bila kuingiliwa na mamlaka yoyote.

Mhadhiri mstaafu wa vyuo vikuu nchini ambaye ni mbobezi wa uhandisi wa teknolojia, Dk. Kamugisha Byabato, alisema matokeo hayo yanatoa tafsiri ya haja ya kuandika Katiba Mpya.

"Tuangalie mchakato mzima na msingi wa tatizo la kikatiba lililoko nchini na mapendekezo ya tume zilizowahi kuundwa na kuleta mapendekezo ya namna ya kuongoza vyama vingi, tukianza na ile ya Jaji Francis Nyalali, mwaka 1992," alisema.

Dk. Byabato alisema ushindi wa CCM ni mwendelezo wa kilichotokea mwaka 2019 na kwamba ni taswira ya kitakachotokea uchaguzi ujao.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya, alisema chama hicho kinaendelea kufanya tathmini ya uchaguzi huo.

Msimamizi wa Uchaguzi Manispaa ya Shinyanga, Alexius Kagunze, alisema uchaguzi katika manispaa hiyo umefanyika kwa huru na haki na kukanusha madai ya kuwapo kwa kura feki.

Alisema alichokibaini ni kwamba vyama vya upinzani havikujipanga vyema kushiriki uchaguzi huo, sababu hata baadhi ya vituo vya kupigia kura hapakuwa na mawakala wao.

Alisisitiza kuwa wagombea wote waliotangazwa kushinda wameshinda kihalali.

**Imeandaliwa na Restuta James, Joyce Lameck (DAR), Paul Mabeja (DODOMA), Marco Maduhu (SHINYANGA) na Mary Mosha (Moshi)**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mikakati, mbinu vinahitajika mapambano dhidi ya Ukimwi

**LEO** ni Siku ya Ukimwi Duniani. Nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN) kupitia Shirika la Afya Duniani (WHO), zinaungana na washirika na jamii katika kuadhimisha siku hiyo ikiwa ni sehemu ya kutafakari ukubwa wa tatizo hilo na kukumbushana hatua za kuchukua katika kupambana na janga hilo ambalo limesababisha mamilioni ya watu duniani kupoteza maisha huku mamilioni wengine wakiishi na virusi vya ugonjwa huo.

Kupitia kaulimbiu ya mwaka huu isemayo "Chukua Hatua Sahihi, Afya Yangu, Haki Yangu", WHO inatoa wito kwa viongozi duniani ma wananchi kuongeza hamasa kuhusu haki ya kupata huduma za afya kwa kuainisha mambo yasiyo ya usawa ambayo ni kikwazo katika kutokomeza Ukimwi.

Aidha, wakati maadhimisho hayo yakifanyika, wito mkubwa unaotolewa ni kuongeza kasi ya mapambano kwa kuwezesha wale wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU) kupata tiba ikiwa ni kutimiza moja ya Malengo Endelevu ya Dunia (SDG) la kumaliza ugonjwa huo ifikapo mwaka 2030.

Katika kutimiza lengo hilo, WHO pia inahimiza kuwapo kwa mikakati endelevu kuhakikisha kila mdau anashiriki katika mapambano dhidi ya ugonjwa huo ikiwamo kuondoa unyanyapaa na kuhakikisha waliogundulika na tatizo hilo wanapatiwa matibabu.

Wakati maadhimisho hayo yakifanyika, tatizo hilo linaonekana kuwa bado kubwa duniani, Afrika na Tanzania ikiwamo. Kwa mujibu wa taarifa za hivi karibuni, maambukizi ya VVU ni makubwa miongoni mwa vijana. Inakadiriwa kuwa takriban watu milioni 1.7 nchini wanaishi na VVU huku mkoa wa Njombe ukiongoza.

Aidha, maambukizi ya ugonjwa huo kwa mwaka ni wastani wa watu 60,000 kwa mujibu wa mwaka 2022 huku asilimia 81 ya waliobainika kuwa na maambukizi wakipata dawa za kufubaza virusi (ARV). Pia imebainika kuwa wanawake na vijana hasa wa kike wenye miaka 15 na kuendelea, wana kiwango kikubwa cha maambukizi.

Pamoja na taarifa zilizotolewa hivi karibuni kuonyesha kuna kushuka kwa maambukizi ya VVU nchini, bado kuna umuhimu mkubwa wa kuongeza nguvu katika mapambano dhidi ya janga hilo.

Elimu kwa umma inapaswa kuendelea kutolewa kwa makundi mbalimbali hasa ya vijana na wanawake ambao wako katika hatari kubwa ya kuambukizwa.

Vijana wa miaka 15 hadi 49 ndio wanaoelewa kuwa wana asilimia kubwa ya maambukizi, hivyo ni muhimu kuongezwa kwa jitihada za kupambana na maradhi hayo.

Msisitizo unapaswa kuwapo kwa kundi hilo kutokana na ukweli kwamba ndilo nguvu kazi ya taifa. Hii ina maana kwamba iwapo hakutakuwa na mkazo mkubwa, kuna hatari ya taifa kukosa nguvu kazi.

Sambamba na elimu, mkazo zaidi unapaswa kuwekwa kwa watu kupima kwa hiari ili kubainika kama wana maambukizi ili kuanza kutumia ARV na kuongeza zaidi muda wa kuishi na kuendelea na majukumu yao ya kila siku.

Kupima na na kuanza matibabu mapema kunasaidia watu wengi kuendelea kuishi kwa tahadhari na kujiepusha na maambukizi mapya.


Kwa kuwa kundi la vijana liko katika hatari zaidi, ni vyema wadau wa afya wakatilia mkazo zaidi kwa kuwaelimisha kuhusu hatari ya ugonjwa huo.

Elimu inapaswa kutolewa katika shule na vyuo vya elimu ya juu ambako kuna hatari ya maambukizi makubwa.

Vijana katika maeneo hayo wanakuwa hatarini kupata maambukizi kwa sababu ya kuwa na tamaa ya kupata vitu vizuri. Pia huko ndiko ambako watu wazima huwafuata na kuwashawishi kushiriki nao ngono zembe ambazo huchangia ongezeko la maambukizi ya VVU,

Nguvu ya pamoja inahitajika katika kupambana na VVU na Ukimwi. Kama ilivyokuwa kaulimbiu wakati wa serikali ya awamu ya nne, Tanzania bila Ukimwi inawezekana.

Kila mmoja achukue hatua.




Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

## Muungwana Lazima Nilonge



# Mliochaguliwa serikali za mitaa anzeni na kero hii maeneo yenu

Na Sabato Kasika

**UCHAGUZI** wa viongozi wa serikali za mitaa umemalizika ukiwa umeacha vilio kwa wagombea wa vyama vya upinzani wakidai kufanyiwa rafu ambazo zimewanyima ushindi.

Pamoja na hayo lengo langu si kutaka kuzungumzia rafu hizo bali kuwataka waliochaguliwa kushirikiana na wananchi kuleta maendeleo katika mitaa yao.

Ninaeleza hivyo kwa sababu wakati wa kampeni wananchi walikuwa wakiwahoji wagombea kuwa ni maendeleo gani wameleta miaka mitano iliyopita hasa kwenye kero ya ukosefu maji na sasa wanataka wachaguliwe tena.

Swali hilo lilionekana ni mwiba kwa wagombea na hivyo kulazimika kulikwepa kwa kuwa baadhi yao hawakuwa na majibu sahihi ya kuwapa wapigakura.

Lakini pamoja na hayo, tayari wamechaguliwa, jambo la msingi ni kuangalia ni wapi walikosea ili warekebishe na kufanya vizuri kazi ambayo wameiomba.

Ukiangalia mitaa mingi haina huduma muhimu za jamii kama maji ambayo kimsingi inapaswa kuwa ya kwanza kuliko vingine, lakini baadhi ya mitaa huduma hiyo inapatikana kwa shida.

Kwenye serikali za mitaa huwa kuna kamati mbalimbali ikiwamo ya maji, kamati hiyo ikiundwa, ifanye kazi usiku na mchana kuhakikisha wananchi wanapata huduma hiyo.

Nitolee mfano mtaa ninaoishi wa King'azi B, Kata ya Kwembe Dar es Salaam, ingawa baadhi ya miji ina mabomba ya maji, lakini hayatoki, kama yakibahatika kutoka, basi ni siku moja tena kwa muda mfupi.

Maana yake ni kwamba hayatoshelezi, hivyo kero hiyo ya muda mrefu ingekuwa ya kwanza kutatuliwa na kamati ya maji ya mtaa ili kuwajengea imani wananchi kuwa serikali yao ya mtaa ipo pamoja nao.

Fikiria kipindi cha joto kali la Dar es Salaam halafu watu hawapati huduma ya maji ya uhakika serikali ya mtaa ipo, kwa nini isifuatilie DAWASA kujua chanzo cha tatizo?

Vilevile, kamati ya maji ya mtaa ifuatilie kujua kwa nini wananchi wanaomba kufungiwa mabomba ya maji halafu hilo halifanyi? Kwa nini baadhi ya watu ameungiwa na wengine hawajaungiwa?

Sina maana kwamba waliofungiwa wanapata huduma hiyo, bali ni kwamba wasio na mabomba na walionayo, wote wanapata huduma ya maji kwa shida.

Kama kwenye kampeni mmeahidi kutatua kero hiyo, hebu itatueni. Kero zipo nyingi, lakini ya ukosefu wa maji ni miongoni mwa kero kubwa katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es Salaam na kwingineko.

Kampeni zimefanyika zikahitimishwa na uchaguzi uliowapa ushindi, hivyo sasa ni wakati wa kutumiza ahadi zenu mlizozitoa kwa wapigakura.

Mmejinadi majukwaani kwa mbwembwe, ninadhani sasa kinachotakiwa ni kuutumikia umma kwa kushirikiana nao kuleta maendeleo kutegemea mahitaji ya maeneo husika.

Lakini ninaamini huduma bora ya maji ni hitaji kubwa la wananchi, yasiwe maji ya kupatikana kwa 'kubipu'. Waliopewa jukumu kusimamia upatikanaji wa huduma ya maji waambiwe ukweli kuwa wanasababisha kero kwa wananchi.

Kwenye baadhi ya maeneo huduma hiyo haijulikani itapatikana lini, kwani sehemu nyingine yanaweza kutoka usiku wa manane wakati watu wamelala na kujikuta wakiyakosa, kwa sababu yanatoka kwa muda mfupi na kukatika.

Iwapo viongozi wapya wa serikali za mitaa kwa kushirikiana na kamati za maji ya mitaa watavalia njuga tatizo hilo, watakuwa wamesaidia kupunguza kero kama sio kuimaliza kabisa.

Wakati mwingine wasimamizi wa utoaji huduma ya maji kwa jamii wanaweza kuzembea baada ya kuona hakuna anayewafuatilia. Hivyo, wajumbe wa kamati za maji za mitaa ziwafutilie.

Binafsi nilishawahi kuwapigia simu kuuliza kulikoni maji yanatoka muda mfupi hayana presha kisha yanakatika kabla wananchi wengi hawajapata huduma hiyo.

Lakini jibu lililotolewa ni kwamba tatizo hilo linafuatiliwa, lakini hadi leo hali hiyo inaendelea. Hivyo, ninadhani kazi ya kwanza mkiingia ofisini iwe ni kutatua keto ya maji kwa kuwafuatilia DAWASA kujua kuna tatizo gani hadi wananchi hawana huduma ya uhakika ya maji.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Pongezi CCM ushindi Serikali za Mitaa



Pascal Mayalla

UCHAGUZI wa serikali za mitaa umekwisha na katika makala hii nimeamua kukipongeza Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kuibuka na ushindi wa kishindo katika kinyang'anyiro hicho. Pia ninawapa pole vyama vya upinzani kwa kushindwa ni lazima wakubali kwamba asiyekubali kushindwa si mshindani.

Katika uchaguzi huo, nafasi za wenyeviti wa vijiji,

CCM imeshinda vijiji 12,150 sawa na asilimia 99.01 huku wapinzani wakishinda vijiji 121 sawa na asilimia 0.09. Tukilinganisha na matokeo ya 2019, japo CCM ndiyo mshindi wa jumla, ukweli ni kwamba CCM imepoteza vijiji 121 ilivyokuwa inavishikilia.

Kwa nafasi za wenyeviti wa mitaa,

CCM imeshinda mitaa 4,213 sawa na asilimia 98.83 na wapinzani mitaa 50 sawa na asilimia 1.17. Aidha kulinganisha na matokeo ya 2019, ukweli ni kwamba CCM imepoteza mitaa 50 iliyokuwa inaishikilia.

Pia katika nafasi za wenyekiti wa vitongoji,

CCM imeshinda vitongoji 62,728 sawa na asilimia 98.26 na wapinzani 2,000 sawa na asilimia 1.74. CCM pia imepoteza vitongoji 2,000 ilivyokuwa inavishikilia.

Kwa nafasi za wajumbe wa halmashauri za vijiji,

CCM imeibuka na ushindi wa 229,075 sawa na asilimia 99.31 wakati wapinzania wameambulia nafasi 1,580 sawa na asilimia 0.69. CCM pia imepoteza viti 1,580 za wajumbe kulinganisha na mwaka 2019.

Katika nafasi za wajumbe wa kamati za mitaa, CCM imeshinda nafasi 21,148 sawa na asilimia 99.30 huku wapinzani wakiambulia nafasi 150 sawa na asilimia 0.70. Wapinzani wamechukua nafasi hizo zilizokuwa zikishikiliwa na CCM katika uchaguzi uliopita.

Ushindi wa jumla wa CCM ni nafasi 329,314 na imepoteza nafasi 3,901 ambazo zimenyakuliwa na upinzani, hivyo kwenye wale waliopata na kupoteza, CCM imepoteza kulinganisha na uchaguzi wa mwaka 2019.

Katika uchaguzi wa mwaka 2019, kila aliyesimamishwa na CCM alishinda. Hiyo inaonesha kuwa ikitolewa elimu ya kutosha ya uraia, mtindo wa Watanzania kuchagua kwa mazoea tu utapungua.

Watu watajengewa uwezo wa kuchagua kwa kufanya kitu kinachoitwa 'informed decisions', hivyo uchaguzi mkuu wa 2025 wapinzani wakisimamisha wagombea wazuri kuliko wa CCM kwenye ubunge na udiwani, watawachagua, hivyo kupata tena Bunge lenye kambi ya upinzani hatimaye kuisimamia serikali kikamilifu.

Nitoe pongezi kwa CCM, chama kubwa, chama bingwa kwa ushindi mkubwa wa kushinda nafasi 329,314 kilioupata katika uchaguzi huu. Lakini pia nitoe pole kwa CCM kupoteza nafasi 3,901 ambazo zimeshikwa na upinzani na kutoa pole kwa upinzani kushindwa na CCM.

Lakini pia pongezi upinzani kuwapokonya CCM nafasi 3,901 ambazo ilikuwa inazishikilia. Kushinda ni kushinda tu na kuna raha yake. Pia kushindwa ni kushindwa, kuna maumivu yake. Hongereni CCM na wapinzani kwa kushinda. Wote mmeshinda. Pia poleni CCM na wapinzani kwa mlichopoteza kwa kuwa wote mmeshinda na mmeshindwa.

Nitoe pongezi kwa vyama vyote vilivyoshiriki uchaguzi huu vizuri kwa kunadi sera zao na kufanya kampeni za kiungwana na kistaarabu. Pia nitoe pole kwa rabsharabsha na maafa yaliyotokea, ukiwamo uvujaji wa machozi, jasho na damu.

Nisiwe mtovu wa shukrani kwa kidogo ili tupatiwe kikubwa japo mpaka sasa bado sijajua kilitokea nini kwenye sheria mpya ya uchaguzi. Sheria hiyo iliifuta Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na kuunda sheria moja ya uchaguzi chini ya Tume huru ya Uchaguzi.

Kwanza nitoe pongezi za dhati kwa kiongozi wetu mkuu, Rais Samia Suluhu Hassan kutupatia sheria mpya ya uchaguz. Kwa vile Rais Samia si mwanasheria, naomba niendelee kumsisitizia kuwa hii sheria yetu mpya ya uchaguzi ni batili, inakwenda kinyume cha katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tasnzania. Naomba tuirekebishe kabla ya uchaguzi mkuu wa 2025.

Pia tushukuru kwa Tume Huru ya Uchaguzi. Watanzania walitaka tume huru na shirikishi ya uchaguzi. Tume iliyoanzishwa, kwa mtazamo wangu, badi ni tume ile ile, ila jina ndio limebadilishwa kuitwa tume huru, Watanzania hatukutaka mabadiliko ya jina la tume kutoka Tume ya Uchaguzi kuwa Tume Huru ya Uchaguzi. Tunaomba mabadiliko ya tume kuwa tume huru na shirikishi ya uchaguzi.

Nashauri tutumie kasoro tulizoziona kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa kama shamba darasa la uchaguzi ujao. Nikisisitiza elimu ya uraia kutolewa kikamilifu. Nikiwa ni mmiliki wa kampuni ya uaandaaji wa maudhui, kutokana na nguvu ya mitandao ya kijamii, hakuna sababu ya kusubiri vipindi virushwe kwenye TV au redio. Kila mwenye uwezo wa kutoa elimu ya uraia, atoe na kuisambaza kupitia mitandao ya kijamii ili kufika mwaka 2025, elimu ya uraia iwe imeenea.

Japo ukuaji wa demokrasia ni mchakato, naendelea kusisitiza CCM na serikali yake ina wajibu wa kulea vyama vya upinzani ili vikue na kujenga demokrasia ya kweli. Watanzania ni wamoja na tunajenga nyumba moja, hivyo hakuna sababu ya kugombea fito. Uchaguzi umekwisha sasa kazi ni moja, kujenga nchi.

**Mungu Ibariki Tanzania.**

**Paskali**
**+255 754 270403**

KONA YA AFYA

# Namna ya kukabiliana na tatizo la nguvu za kiume



Na Dk. Mabula Budodi

KWA sasa sina raha kabisa daktari." Ilikuwa kauli ya mgonjwa akimweleza daktari baada ya kufika hosipitalini.

"Si kama mwanzo tena ilivyokuwa kipindi nakutana na mke wangu. Nimekuwa napata lawama sana kutoka kwa mke wangu takribani miaka miwili sasa hadi naona ni hakika amevumilia vya kutosha kwa kweli. Nampenda sana mke wangu kusema kweli wala sitaki aniache kwa ajili ya jambo hili ambalo kwa sasa naona kama linakuwa sugu.

"Nilikuwa nadhania atakuwa ana mambo yake binafsi kipindi akiwa ananiambia kuhusu hali yangu ya kushindwa kutoa haki yake ya ndoa. Hata mimi kweli nimeona mabadiliko makubwa sana kutoka kwangu kuhusu tendo la ndoa. Kwa sasa uwezo wangu si kama wa mwanzo tulivyokutana," alibainisha.

Mwanamume huyo alisema ndani ya nyumba kulikuwa hakuna furaha kabisa tofauti na ilivyokuwa awali na kwamba ilifikia hatua ya mke wake kuomba talaka kwa sababu ameshaongea sana na anaona hatilii maanani tatizo hilo. Alisema ndani ya nyumba kila siku ilikuwa ugomvi. Hali hiyo ilianza polepole kwa kutoa huduma ya unyumba kidogo lakini ilifikia hatua ya kukosa kabisa uwezo wa kufanya tena tendo hata akijitahidi namna gani.

"Mara ya kwanza nilijua labda ni uchovu wa kazi tu lakini hata siku nyingine nikiwa niko nyumbani tu, nakuwa vilevile, siwezi tena kumfikisha au kumridhisha mke wangu. Sijui tatizo limeanzia wapi, kwa kuwa zamani nilikuwa napenda kufanya mazoezi, lakini nakosa muda na hii itakuwa imechangia licha ya kwamba sina uhakika," alisema.

Kwa mujibu wa mwanamume huyo, miaka mitatu au minne iliyopita aligundulika kuwa na tatizo la sukari huku shinikizo la damu likimnyemelea, ndipo daktari alipomshauri afuatilie tatizo kwa kupima mara kwa mara na kubadilisha mfumo wa maisha kama vile kuacha kuvuta sigara na kunywa pombe.

Baada ya daktari kumsikiliza kwa makini na kumpa ushauri, alianza matibabu baada ya kugundulika kuwa na tatizo la sukari na shinikizo la damu kwa muda mrefu ambalo alizembea kufuatilia vizuri.

Tatizo hilo, alisema lilionekana kuchangiwa na unywaji pombe na uvutaji wa sigara, hivyo akashauriwa aache vyote na kuanza matibabu. Baada ya muda mfupi, alisema alianza kuona mabadiliko.

UKUBWA WA TATIZO

Tatizo la nguvu za kiume limekua linalokuwa kwa kasi sana duniani. Limechangia kuongezeka kwa matumizi ya dawa za kuongeza nguvu za kiume kwa kutumia dawa za kienyeji na hosipitalini ili kupata ahueni.

Yote hiyo imesababishwa na kushidwa kujiuliza chanzo ni nini na hatimaye kupunguza au kumaliza tatizo.

Takwimu zinaonesha kuwa tatizo la nguvu za kiume linakadiriwa kudhuru takribani watu milioni 332 ifikapo mwaka 2025. Chanzo kikubwa cha tatizo hilo ni magonjwa yasiyo ya kuambukiza kama vile kisukari, shinikizo la damu, msongo wa mawazo, uvutaji wa sigara na unywaji wa pombe.

Utafiti mdogo uliofanyika Kinondoni, Dar es Salaam na kuchapishwa katika jarida la BMC mwaka 2016 ukihusisha wanaume 441 wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea, ulionesha kwamba tatizo la nguvu za kiume limeonekana zaidi katika watu wa umri wa wastani wa miaka 47.1. asilimia 57.6 walionekana kuwa na uzito uliopitiliza, asilimia 8.2 wakiwa na kisukari na asilimia 61.5 walikuwa na tatizo la shinikizo la damu.

Aidha, kati ya watu hao, 106 walionekana wakiwa na tatizo la nguvu za kiume sawa na asilimia 24.

Pia katika utafiti huo, watu waliokuwa na zaidi ya miaka 55 walionekana wakiwa na historia ya uvutaji wa sigara, kisukari na shinikizo la damu. Pia wenye umri wa miaka 40 na kuendelea walionekana kuwa na tatizo la kisukari ambalo lilikuwa likichangia moja kwa moja kuwapo kwa tatizo hilo.

Utafiti uliofanyika Moshi, Kilimanjaro na kuchapishwa katika jarida la PMC mwaka 2020 ukihusisha watu 381 unaonesha ukubwa wa tatizo. Utafiti ulionesha kuwa mtu mmoja kati ya watatu alikuwa na tatizo la nguvu za kiume.

Kisukari na shinikizo la damu husababisha tatizo la nguvu za kiume kwa kuharibu mishipa ya damu na mishipa ya fahamu ambayo hupeleka fahamu na damu kwenye mfumo wa uzazi, hivyo kufanya kushindwa kufanya kazi vizuri.

Ili kukabiliana na tatizo hilo, ni muhimu kufuatilia matibabu ya sukari na shinikizo la damu. Hii itasaidia kupunguza tatizo hili kwa kiasi kikubwa. Pia ni vizuri kuacha uvutaji wa sigara na kunywa pombe, vitu ambavyo pia huchangia kusababisha madhara kuwa makubwa zaidi.

Pia inashauriwa mtu kufanya mazoezi ili kuimarisha uzalishaji wa homoni aina ya 'testosterone' ambazo huchangia kuboresha nguvu za kiume na kupunguza uzito uliopitiliza.

**•Dk. Budodi ni daktari wa binadamu. Anapatikana kwa namba 0710 980096na baruapepe mabulabudodi@gmail.com**

# Watoto 180 waokolewa ndani ya siku sita kabla kukeketwa

**Na Grace Mwakalinga**

JESHI la Polisi katika mkoa wa kipolisi wa Tarime/ Rorya ndani ya siku sita limeokoa zaidi ya watoto wa kike 184 walioandaliwa kukeketwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Polisi nchini, Naibu Kamishna (DCP) David Misime, watoto hao wameokolewa na jeshi hilo kwa kushirikiana na wadau wengine katika Mkoa wa Kipolisi wa Tarime Rorya.

Alisema watoto hao wameokolewa ndani ya siku hizo tangu kuanza Maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, yaliyoanza Novemba 25 mwaka huu. DCP Misime, alisema watoto hao waliandaliwa kukeketwa mwezi ujao na sasa wamehifadhiwa sehemu maalum wakati hatua za kisheria zikiendelea.

"Jeshi la Polisi limeamua kuadhimisha siku 16 Tarime Rorya ambapo maofisa, wakaguzi na askari wengine wanaofanya kazi katika madawati ya jinsia ya watoto nchini, wakaguzi wa kata wameweka kambi huko," alisema DCP Misime.

Alisema shughuli wanazifanya ni kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji dhidi ya watoto, ili wazazi watambue madhara ya ukeketaji, watashirikiana na viongozi wa dini, mitaa, kimila wazazi na makundi mengine kusaidia kuvizuia.

"Tunatoa rai kwa wananchi wote kutumia maadhimisho haya kushirikiana kwa dhati ili kutokomeza vitendo vya ukatili wa kijinsia ," alisema DCP Misime.



Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Uongozaji Ndege katika Mamlaka ya Usafiri wa anga Tanzania (TCAA), Flora Alphonce, akipokea tuzo ya mshindi wa tatu kwa upande wa mamlaka za udhibiti katika uandaaji wa taarifa za fedha ya mwaka 2023 kutoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali, CPA. Benjamin Mashauri, wakati wa hafla ya utoaji tuzo kwa taasisi, makampuni pamoja na mashirika zinazotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) Dar es Salaam juzi. **PICHA: MOSHI LUSONZO**

# TRA mshindi tuzo NBAA

**Na Thobias Mwanakatwe**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) imeibuka mshindi wa jumla katika uandaaji wa hesabu za kifedha zinazozingatia viwango vya kimataifa vya uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na Sekta za Kibiashara (IFRS).

Pia imeibuka mshindi wa kwanza katika kipengele cha Taasisi za Serikali (Government Agency Categories) katika tuzo hizo ambazo zimetolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Akizungumza jana baada ya kupata tuzo hizo, Naibu Kamishna Mkuu wa TRA, Mcha Hassan, alisema tuzo hizo ni uthibitisho wa dhamira ya TRA ya kuhakikisha uwazi, uwajibikaji na weledi katika matumizi sahihi ya viwango vya juu vya kitaalamu katika uandaaji na uwasilishaji wa taarifa za kifedha.

Mcha alisema TRA ina watumishi wenye weledi wa kutosha katika usimamizi bora wa kifedha na uandaaji wa taarifa zinazozingatia viwango vya kimataifa.

"Tuzo hizi ni uthibitisho kuwa TRA tuna watumishi wenye weledi katika kusimamia, kuandaa na kuwasilisha taarifa za fedha kwa kuzingatia viwango vya kimataifa," alisema.

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA) imekuwa ikiandaa tuzo kila mwaka kwa waandaaji wa taarifa za kifedha zinazozingatia viwango vya kimataifa vya Uhasibu katika Sekta ya Umma (IPSAS) na Sekta za Kibiashara (IFRS).

Tuzo hizo za uwasilishaji wa taarifa za kifedha kwa mwaka 2023 zimetolewa juzi Bunju, Dar es Salaam.

# Vijana wapongezwa kushinda uchaguzi S/Mitaa

**Na Mwandishi Wetu,**
MOROGORO

RAIS wa Jumuiya ya Wanafunzi Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (TAHLISO), Zainab Kitima, amewapongeza vijana wote waliojitokeza kugombea na kushinda nafasi za uongozi wa Serikali za Mitaa katika uchaguzi uliofanyika Novemba 27, mwaka huu.

Kitima alitoa pongezi hizo jana akiwa mjini hapa, ikiwa ni siku ya pili baada ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mohamed Mchengerwa kutangaza matokeo ya jumla ya uchaguzi huo.

"Ninawapongeza vijana waliojitokeza kupiga kura na kugombea nafasi za uongozi wa Serikali za Mitaa katika maeneo mbalimbali nchini, hakika wametimiza haki yao ya kikatiba," alisema.

Kitima aliwataka vijana wote ambao wameaminiwa na wananchi na kuchaguliwa katika nafasi mbalimbali za uongozi wa serikali za mitaa kuhakikisha wanawatumikia wananchi kwa uadilifu na weledi ili kuwaletea maendeleo.

Aliongeza kuwa katika uchaguzi wa mwaka huu, vijana wengi walijitokeza kugombea nafasi za uongozi ndiyo maana wameshinda tofauti na awali ilipokuwa inaaminika kwamba nafasi za uongozi wa serikali za mitaa ni kwa ajili ya wazee.

"Mwaka huu tumeona vijana wasomi wamegombea nafasi za ungozi wa serikali za mitaa na kushinda kwa kishindo, hivyo naishukuru jamii kwa kuwaamini vijana ili wapate fursa ya kutumia elimu yao katika kuwatumikia," alisema.

Sambamba na hilo, Kitima alipongeza serikali kwa kuhakikisha uchaguzi wa mwaka huu unakuwa huru na wa haki, licha ya kuwepo na dosari chache zilizoripotiwa kwenye maeneo kadhaa ambazo haziwezi kukosekana katika nchi yoyote ya kidemokrasia.

Pia aliipongeza serikali kwa kuvishirikisha vyama vyote vya siasa katika hatua na mchakato mzima wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu.

Wananchi 26,963,182 walipiga kura katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu uliofanyika Novemba 27, 2024.

# MAISHA

DESEMBA 1, 2024

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13


## Mwendo wa ng'ara ng'ara



Ukurasa 15


## MAISHA NI NYUMBA

Rembesha uzio kupendezesha nyumba yako



## HARUSI


Ukurasa 12



# Urembo wa uso, nogesha na ndizi

Ukurasa 14

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | 3 | 2 | 1 |
| 2 | 1 | 4 | 3 |
| 3 | 4 | 1 | 2 |
| 1 | 2 | 3 | 4 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| A | ■ | S | ■ | B |
| U | M | E | M | E |
| ■ | ■ | H | ■ | I |
| U | ■ | E | ■ | ■ |
| J | A | M | B | O |
| I | ■ | U | ■ | A |

## AMSHA AKILI

HAYA WADOGO ZANGU, TUENDELEE NA AMSHA AKILI IITWAYO SUDOKU. JAZA NAMBA MOJA MPAKA NNE KWA KILA MSTARI IWE KUTOKA CHINI MPAKA JUU AMA KUSHOTO KWENDA KULIA. HAKIKISHA NAMBA ZINAZOFANANA HAZIGONGANI KATIKA MSTARI MMOJA. KAZI KWAKO!

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4 | | | |
| 2 | | 4 | 3 |
| 3 | | | |
| 1 | | | |


## FUMBO TOTO

Ingiza majina ya wanyama kwa Kiingereza katika vyumba husika.

1.CHUI 2.MBUZI 3.MWEWE
4.PANYA 5.KUKU 6.NJIWA


| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | 2 | | | ■ |
| ■ | ■ | | ■ | ■ | ■ |
| ■ | 3 | | | | ■ |
| 4 | | | ■ | ■ | 5 |
| ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| 6 | | | | | |

## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alikuwa akiwinda ndege na wenzake msituni. Walijaribu mara kadhaa kuwanasa ndege kwa kutumia mtego maalum uliokuwa kwenye tundu jipya la kuhifadhi ndege.

**Juma:** Jamani mimi nimechoka, kila ndege tuliyemuwinda hakunasa.

**John:** Tuvumilie tu, watakuja ndege wengine tutawanasa tu

**Juma:** Hapana ndege watakaoingia kwenye mtego watakuwa wajinga.

**John:** Sio hivyo kwani wajanja hawanasi?

**Juma:** Ndio kwa sababu tundu letu ni jipya, si umesikia ule msemo ndege mjanja hunasa kwenye tundu bovu.?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Kupuuzia ndoto za usiku kunavyotesa watu wengi

***KARIBU msomaji wangu kwenye safu yetu hii ya Maisha Ndivyo Yalivyo. Kwa wiki kadhaa tumejadili hapa kuhusiana na hatari ya ndoto tunazoota usiku tukiwa tumelala.***

Nikasema kwamba ulimwengu wa ndoto unaelezewa kuwa ni muhimu kama ulivyo ulimwengu wa damu na nyama. Je, unajua mwanadamu ni matokeo ya ndoto anazoota?

Ndoto ni njia mojawapo ya mawasiliano. Ni hatari kupuuzia ndoto unazoota kwani ndoto ni picha ya maisha yako kwenye ulimwengu wa roho, ambao hauonekani kwa macho.

Ndoto hazidanganyi. Unaweza kushindwa kuielewa ndoto unayoiota lakini ndoto haidanganyi. Ndoto huonyesha maisha yako ya mbele na ya nyuma.

Kila ndoto unayoiota hubeba ujumbe hata kama huelewi kwa wakati huo, maana shetani anapenda sana kufuatilia maisha ya ndoto ya mwanadamu na kupenyeza uovu wake. Upo wakati hujigeuza malaika wa nuru na kuwadanganya watu kupitia ndoto.

Tumeona shuhuda kadhaa za watu walioota ndoto wakapuuzia na matokeo yake kile walichoota kikatokea. Nilitaja shuhuda chache wiki iliyopita, leo nimalizie nyingine kadhaa.

Baba mmoja alipooza baada ya kuota anarushiwa mishale kwenye ndoto. Dada mmoja aitwaye Naomi alikwenda kumuona mtumishi wa Mungu na wakati wa ibada akashangaza na kuacha wengi midomo wazi.

Akasema, mimi huwa naota napakwa kinyesi cha mwanadamu na nikiamka nakuta harufu imesambaa mwili wangu na ugomvi kati yangu na mume wangu huanzia hapo.

Hali hii imefanya niachike mara mbili na sasa tena ile ndoto imeanza tena kunitokea na huyu mume wangu wa tatu anatishia kuniacha kwani anainusa harufu ya kinyesi mwilini. Ninahitaji msaada wa maombi ili hali hii iniachie".

Wakati wa maombi iligundulika kuwa kuna wachawi walikuwa hawataki aishi na mume ndio maana waliamua kumshambulia kupitia ndoto ili anuke na akataliwe. Baada ya maombi alifunguliwa hali ile ikatoweka!

Dada Eva alikuwa na tatizo kubwa la kiuchumi na mafarakano kwenye ndoa. Aliposikia somo la uhusiano kati ya ndoto mtu anazoota na matatizo yako, aliomba kuelezea ndoto zilizokuwa zinamsumbua.

Alisema, "Mimi huwa naota ndoto nasafiri kwa fisi kuelekea kwenye mji fulani kama kuzimu hivi. Nikifika huko napewa kazi ya kupikia watoto wadogo kwenye pipa. Ninakuwa natumia viganja vya mwanadamu kama kuni. Pia naota nimekufa mara nyingi.

Wakati wa maombezi iligundulika kuwa tayari alikuwa ameunganishwa na chama cha wachawi na walikuwa wanamchukua usiku kwenda kufanya kazi zao.

Pia walikuwa wanaharibu biashara zake na kumletea mafarakano kwenye ndoa. Kumbe tatizo lake lilianza zamani na baada ya maombi alifunguliwa na kuwekwa huru!

Dada Leticia alifunga ndoa na mzungu na waliishi miaka kumi bila mafarakano yoyote. Siku moja aliota mwanamke mweupe aliyevaa shela akija kitandani mwake na kumfukuza.

Alipoamka alimsimulia mumewe; mume akamwambia apuuzie hiyo ndoto kwani haikuwa na maana kutokana na kwamba walikuwa wakiishi kwa amani.

Cha kushangaza baada ya miezi sita dada Leticia alifukuzwa na yule mzungu katika mazingira ya ajabu na mwanamke mzungu akachukua nafasi yake. Laiti angejua umuhimu wa kufanya maombi na kufuta hiyo ndoto asingeachika.

Mpenzi msomaji, bila shaka shuhuda hizo zimefungua ufahamu wako kuhusu habari ya ndoto unazoota usiku ukiwa umelala. Hebu sasa tuone tafsiri ya ndoto kadhaa ambazo baadhi ya watu huota usiku.

Unaota unachanjwa chale kwenye ndoto, inamaanisha kuna maagano ya kuzimu yanafanywa juu yako kwenye ulimwengu wa roho. Unaota umefunga ndoa na mtu usiyemjua. Maana yake ndoto hii itakufanya usioe/usiolewe na kama upo kwenye ndoa uachike.

Unapakwa kinyesi mwilini na mtu/watu kwenye ndoto. Inamaanisha unapandikizwa roho ya mikosi na balaa na roho ya kukataliwa.

Ukiota unang'olewa meno hasa ya mbele, ujue kuwa wachawi wamekusudia kuua nguvu zako kiroho. Kunyolewa nywele kwenye ndoto maana yake utukufu wako unachukuliwa kwani nywele ni ishara ya utukufu!

Unaongea na ndugu zako waliokufa kwenye ukoo. Inamaanisha unafuatiliwa na mizimu ya ukoo. Unaota uko uchi, inamaanisha shetani amekusudia kukuaibisha na kukushushia heshima yako.

***Umelazwa hospitali, inamanisha roho ya maradhi inakunyemelea. Unaota unakula matapishi yako inamaanisha unarudia makosa ya zamani. Je, una maoni, kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi

# Wanyama wafugwao wametuzidi akili kulea watoto

KAMA taifa hatujafanya utafiti wa kutosha kuhusu 'day care centers' (vituo vya kulea watoto) licha ya kwamba katika kipindi cha maendeleo ya awali ya mtoto, elimu kwa watoto wadogo wenye umri wa miaka sifuri hadi miwili ni muhimu sana.

Katika hatua hii, mtoto anajenga misingi ya kukua kihisia, kujenga lugha na kujiendeleza kijamii.

Ingawa vituo hivi vinavyojihusisha na malezi ya watoto vimekuwa na wateja, bado kuna changamoto ya usalama na ustawi wa wanaohudumiwa.

Kuku analea watoto wake, bata analea watoto wake, nyani anawalea watoto wake, hata mbuzi na ng'ombe wanalea watoto wao lakini imekuwa ngumu kwa binadamu.

Tusije tukaachia wanyama wafugwao wasio na akili kulea, halafu sisi wenye akili ya kulea na tulioumbwa kwa mfano wa Mungu, tukaacha kuwalea watoto wetu katika njia itupasayo.

Tukawaacha watoto wetu tukabaki tukikimbizana na maisha, kutafuta mshiko, bahasha. Ni lazima mzazi au mlezi, utenge muda wa kulea mtoto wako.

Katika mijadala mingi, wazazi na wataalamu wa malezi wanakubaliana kuwa talaka inaweza kuwa na athari kubwa kwa watoto.

Watoto wanapitia mabadiliko makubwa katika mazingira yao ya nyumbani, ambayo yanaweza kusababishia msongo wa mawazo na huzuni. Wakati mwingine hata matatizo ya kiakili na kihisia.

Kumekuwa na malalamiko, majadiliano na utafiti mbalimbali kuhusu ongezeko la hali ya mmonyoko wa maadili na talaka. Vyote hivi vimekuwa sehemu ya kuongeza hatari ya watoto kupata matatizo ya afya ya akili. Watoto wanapogombana zingatia kujua chanzo cha ugomvi.

Wakati mwingine, ugomvi husababishwa na upendeleo wa mzazi kwa mtoto mmoja.

Upendeleo wa mzazi kwa mtoto mmoja, ni suala linaloweza kusababisha mgawanyiko wa kihisia na changamoto za uhusiano katika familia.

Hali hii hutokea pale mzazi anapoonesha upendo, uangalizi au msaada wa kipekee kwa mtoto mmoja huku mwingine aa wengine wakiachwa

Mwambie mtoto kwamba ni sawa kubadilisha mtazamo wake akigundua mawazo mapya au anapoona umuhimu wa kufanya hivyo.

Nimewaza kwamba hivi ni njia gani itumike kutatua changamoto ya wazazi wengi kushindwa kukea watoto na kutumia muda mwingi kukimbilia kutafuta maisha?

Nikapata majibu kwamba changamoto ya wazazi wengi kushindwa kukea watoto kutokana na majukumu ya kutafuta riziki ni ya kawaida katika jamii nyingi. Hata hivyo, kuna njia kadhaa zinazoweza kusaidia kutatua changamoto hii.

Huduma za malezi na ushauri kwa wazazi. Serikali na mashirika ya kijamii yanaweza kuanzisha programu za kutoa elimu na ushauri kwa wazazi kuhusu umuhimu wa malezi bora na muda wa kutosha wa kuwa na watoto.

Hii inaweza kujumuisha mafunzo kuhusu jinsi ya kupanga ratiba ya familia na kutafuta mbinu bora za kushirikiana katika malezi, hata kama mmoja wa wazazi anakuwa na kazi nyingi.

'Flexibility' haina budi kuwapo kazini. Waajiri wanaweza kuanzisha saa za kazi za mbali (remote work) au kubadili ratiba ili wazazi wapate muda wa kutosha wa kuwa na familia na watoto.

Hii itasaidia kupunguza mzigo wa kazi na kuwawezesha wazazi kushiriki kikamilifu katika malezi.

Usaidizi kutoka kwa jamii pia ni muhimu Familia, marafiki, na majirani wanaweza kusaidia kutoa msaada kwa wazazi.

Wazazi wanaweza kushirikiana ili kusaidiana na kulea watoto, kwa mfano, wakati mzazi mmoja anapokuwa na kazi ndefu au ana majukumu mengine.

Mbinu za kijamii na teknolojia zinaweza kusaidia familia. Programu kama vile huduma za day care au huduma za malezi kwa kutumia teknolojia (apps za malezi), zinaweza kuwa suluhisho bora kwa wazazi wenye kazi ngumu.

Teknolojia pia inaweza kusaidia wazazi kuungana na familia na kuwatunza watoto kwa njia bora, kama vile kutumia video calls na shughuli za mtandaoni ili kuweka uhusiano mzuri na watoto.

Kuelimisha jamii kuhusu usawa wa kijinsia. Ni muhimu kuhamasisha usawa kati ya baba na mama katika majukumu ya malezi.


Wazazi wote wawili wanapaswa kuchukua jukumu la kutosha katika kulea watoto, badala ya mzigo kuwa juu ya mama pekee.


Hii itasaidia kupunguza mzigo kwa mmoja wa wazazi na kuwezesha wote kushiriki katika malezi.

Kwa kutumia mbinu hizi, wazazi wataweza kupunguza changamoto ya kushindwa kukea watoto, hata wakati wanapojitahidi kutafuta maisha.


***• Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com***

# HARUSI
















Ulikuwa waklati wa furaha kwa Prisca Simbeye na Luckest Dude baada ya kufunga ndoa hivi karibuni na kuambatana na sherehe ya aina yake katika ukumbu wa Seabreez, Mbezi Dar es Salaam.

# MITINDO



# Mwendo wa ng'ara ng'ara

KATIKA kipindi cha joto, mavazi mepesi ndiyo yanapendekezwa zaidi ili kuufanya mwili uweze kupumua.

Aina hii ya mavazi yanampa mtu uhuru wa kuvaa mapambo ya kila aina ili kuongeza mvuto katika mwonekano.

Kipindi cha joto mapambo huonekana kirahisi kutokana na nguo zinazovaliwa kuwa nyepesi zaidi.

**MKUFU NA KIDANI**

Unashauriwa wakati wa joto kuvaa mkufu wenye kidani kama mambo kuu, kwani unapovaliwa shingoni huonekana kwa urahisi baada ya eneo kubwa kuwa wazi.



Hauna haja ya kujitanua ili mkufu na kidani uonekane, unachotakiwa kama umevaa shati au fulana yenye vifungo mbele kuachia wazi sehemu kubwa.

Mikufu ya dhahabu na madini mengine huvaliwa sana katika kipindi cha joto, hakika ni wakati wa kuonyesha jinsi gani unajipenda.

**HERENI**

Ukiwa na jozi ya hereni za kila aina, huu ndio wakati wako wa kuchagua zipi unataka kuvaa leo au kesho kwa sababu ni muda sahihi wa kutumia.

Wakati wa joto kwa kawaida watu huacha kichwa kikiwa wazi na hivyo pambo la hereni linaonekana vyema.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# Urembo wa uso, nogesha na ndizi

NDIZI mbivu zina virutubisho muhimu vinavyoboresha ngozi. Ndizi pia zina aina tatu za sukari zinazojulikana kama sucrose, fructose na glucose'.

Leo tutaelezana matumizi sahihi ya ndizi katika urembo wa ngozi ya uso na shingo yako.

Kwanza kabisa hakikisha unanawa uso wako mara tatu kwa siku. Unapofanya hivyo unaondoa uchafu.





**Ndizi pia husaidia kuzuia chunusi.**

Hakikisha unanawa uso kwa sabuni ambayo inaendana na ngozi yako. Ikiwa ngozi yako ni ya mafuta, hakikisha unatumia sabuni ambayo itakuachachukiwa mkavu na kama ngozi yako ina ukavu, jioshe na sabuni itakayokufanya uwe na unyevu.

**Kulainisha ngozi**

Changanya asali na ndizi moja iliyopondwa na upake kwenye uso na shingo. Nawa uso kwa maji ya uvuguvu baada ya muda wa nusu saa. Fanya hivi angalau mara moja kwa wiki.

**Kung'arisha uso**

Ndizi huwa na Vitamin C ambayo husaidia kuiweka ngozi kuonekana iking'aa. Kwenye ndizi iliyopondwa, ongeza vijiko viwili vidogo vya juisi ya limau na upake kwa uso na shingo. Osha kwa maji ya uvuguvugu baada ya dakika 20. Ni vizuri kupaka mchanganyiko huu wakati unapoenda kulala.

**Kuzuia mikunjo**

Ponda parachichi na ndizi pamoja. Paka kwa uso na uoshe baada ya muda. Mchanganyiko huu hulainisha ngozi ya uso na kuwa laini lakini pia hupunguza ukubwa wa matundu ya ngozi ya uso wako.

**Kusugulia uso**

Changanya ndizi na sukari kijiko kimoja, kisha paka usoni na usugue taratibu. Ndizi hulainisha ngozi kavu na sukari huondoa seli zilizokufa kwenye ngozi.

Saga ndizi moja na Oats vijiko vitatu kisha changanya na asali na maziwa. Paka usoni kwa dakika 15 kisha sugua.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Faida za ukwaju mwilini

UKWAJU ni matunda yenye ladha kali ambayo hutumika sana kama kiungo na pia kama tiba asili kwa jamii nyingi za Afrika Mashariki.

Ukwaju una virutubisho mbalimbali kama vile vitamini C, vitamini B, madini kama magnesium, chuma, potassium pamoja na nyuzi nyuzi na vioksidishaji mwilini.

Faida za ukwaju ni chanzo kikubwa cha Vitamini C, husaidia mwili kupambana na maambukizi mbalimbali, kuzuia mafua na kuimarisha ngozi kwa kupambana na mionzi hatarishi ya jua.

Kusaidia kuweka mifupa kutokana na kuwa na madini ya kalsiamu yaliyomo kwenye ukwaju yana mchango mkubwa katika kuimarisha mifupa na meno.

Kuboresha mmeng'enyo wa chakula kutokana na nyuzinyuzi nyingi ambazo husaidia katika mmeng'enyo wa chakula.

Kupunguza uzito kwa sababu ya nyuzinyuzi zilizomo ndani ya ukwaju husaidia mtu kujisikia kushiba kwa muda mrefu na hivyo kupunguza hamu ya kula mara kwa mara.



**Jinsi ya kutumia ukwaju**

Juisi ya ukwaju: Unaweza kutengeneza juisi ya ukwaju kwa kuloweka matunda haya kwenye maji kwa muda, kisha kukamua na kuchuja. Juisi hii ni tamu na yenye virutubisho vingi.

Ukwaju kiungo: Unaweza kuongeza ukwaju katika mapishi mbalimbali, kama vile kwenye michuzi, mchuzi wa nyama, au kwenye wali ili kuongeza ladha.

Kula ukwaju mbichi: Kwa wale wanaopenda ladha ya ukwaju, kula mbichi kunaweza kuwa njia bora ya kupata virutubisho vyote muhimu.

MAISHA NI NYUMBA

Na Restuta James

# Rangi za nyumba zilizotamba mwaka huu

MSIMU pendwa sikukuu za mwisho wa mwaka, umeanza kwa namna yake, baada ya kampuni, mashirika na watu binafsi, kuanza kutoa tathmini zao, kuhusu mwenendo wa mwaka huu 2024.

Kampuni za rangi nazo zimetoa orodha ya rangi zinazovuma 2024, bluu na mchanganyiko wa rangi hiyo ukionesha kuwa kileleni, ikizishinda rangi nyingine.

Pamoja na bluu kuwa kileleni, kuna baadhi ya rangi zinazorudi kutoka miaka ya nyuma, baadhi zimeshuka kabisa kwenye orodha na baadhi ni mpya kabisa.

Wachambuzi wa masuala ya mapambo ya nyumba na ubunifu majenzi, wanaeleza kuwa mchanganyiko wa bluu umeonekana kutuliza nafsi, kuvutia na kuongeza nguvu.

Bluu bahari, bluu tulivu, bluu ya kijivu na bluu ya kijani, ni miongoni mwa rangi kwenye kundi la bluu zilizotamba mwaka huu.


"Inapooanishwa bluu na kijivu (Grey Blue), huunda mwonekano mkali na mzuri, ambao ni chaguo bora kwa nafasi za kisasa na za kitamaduni. Rangi hizi zinatumika kuleta uwepo wa utulivu kwenye chumba chochote," anasema Agnes Massawe, mtaalamu wa rangi.

Anasema kwenye bluu, kuna iliyo 'laini' yaani soft blue inayotokana na mchanganyiko kidogo wa kijivu na bluu, akieleza kuwa inakufanya ujisikie amani na ni rahisi kuangalia.

Nyingine ni bluu ya kijani inayotajwa kuamsha utulivu na kuleta mazingira ya asili kwenye eneo lolote, akitaja jikoni, vyumbani au nje.

Anashauri kwamba rangi hizo ni nzuri zaidi kwenye vyumba, bafu au maeneo ya kupumzika, kwa kuwa zinaongeza utulivu wa nafsi, akili na macho.

Aidha, nyeusi, kahawia na nyeupe, bado zimeendelea kutamba licha ya kwamba zimetawaliwa zaidi na ubluu.



Na Elizabeth Zaya





# Huisha nyumba yako uifurahie

UZIO ni moja ya sura ambazo zinaweza kutumika kama urembo wa nyumba kulingana na namna mhusika anavyotaka uwe kwa kutegemea na bajeti au ubunifu unaotumika kuutengeneza.

Kwa ujumla, nyumba inapozungushiwa uzio iwe ni kwa ajili ya ulinzi, usalama, faragha au muonekano, lakini unasaidia pia kuongeza thamani ya nyumba husika.

Kwa mazingira yetu ya kitanzania zipo uzio za aina mbalimbali ikiwamo za tofali, mbao, miti, makuti, chuma, aluminiam, wavu, bati na nyinginezo.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Stephen Kennedy, anasema yako mambo ya kuzingatia kabla ya kuweka uzio wa nyumba yako.

Anasema ni vyema kuepuka kukurupuka kuchagua uzio kabla hujafahamu gharama za utunzaji wake na kwamba endapo utaamua kimakosa upo uwezekano wa kuharibu muonekano wa sura ya nyumba yako hata kama ni nzuri kiasi gani.

"Kwa mfano unapoweka uzio wa mbao, unatakiwa ujue kwamba unatakiwa kupakwa rangi mara kwa mara na ujue zinaoza pia baadae, kwa hiyo zinahitaji maboresho ya kila mara kwa sababu pasipo kufanya hivyo zinaharibika, hivi ni vitu ambavyo unapaswa kujua katika kila aina ya uzio unaotaka kuweka," anasema Kennedy.


Jambo lingine anasema kwamba kabla ya kutengeneza uzio wako unatakiwa ufahamu unatakiwa uwe kwa mtindo gani.

Anashauri kwamba uzio wa kurembesha zaidi katika lango kuu ikiwamo kuweka taa za rangi unasaidia kuweka muonekano mzuri wa ukuta na nyumba kwa ujumla.

Kennedy anashauri kuweka uzio wenye kuleta faragha na wa kuimarisha ulinzi katika nyumba na siyo bora uzio.

Anasema kwamba uzio unaoacha nafasi au matundu katika nyumba hauna faragha na wala hauwezi kukulinda vya kutosha, ila unakupa starehe ya kuangalia kinachoendelea nje ya makazi yako unapokuwa umejipumzisha.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
ETI ANASEMA ALIJUA KAMA ATASHINDWA ALIGOMBEA NINI?
MBONA SASA ANALIA?
MIE NATAKA NITAFUTE MTU NIOLEWE SASA
UNAWAZIMU! NANI UMUACHE ADANGE PEKE YAKE?
JUKWAANI
NINGESHANGAA NINGESIKIA ETI MIMI NIMESHINDA KURA?
KWA SURA HIYO HATA MIMI PIA NINGESHANGAA!
NA HIYO MIJINO YAKO MTANI DUUU! HAPANA!
WEWE NDIO KIZABIZABINA ULIYENIKOSESHA USHINDI KWENYE UCHAGUZI HUU!
NIMEKUPA HELA UKAWAGAWIE WENYE AKILI UKAENDA KWA WALEVI!
ALIYEKWAMBIA WALEVI HAWANA AKILI NI NANI? STIMU ZAO NDIO ZIMEMCHAGUA MTU SAHIHI
MIE MWENYEWE NIMEKULA HELA ZAKO...KAMA UNAWEZA NJOO TUZIPANGE ZA JUU JUU!
NA UKINIGUSA NAPIGA KELELE UNANIBAKA! JAPO NAPENDA TUZICHAPE
ETI MUME WANGU YUPO KWAKO?
MSUBIRI ANAKOGA KISHA NIMPAKE MAFUTA ALAFU NTAKUPA WENDE NAE
SWAHIBA UCHAGUZI UMEPITA TUNAPITANA KAMA HATUJUANI?
UJUANE NA NANI SURA KAMA ZIRAILI MTOA ROHO!
WEWE FITINA ZA KISIASA UMEZIJULIA WAPI MPAKA UTOKE NISIKUONE NYUMBANI WIKI NZIMA?
UTANIONAJE CHUMBANI KWA MGANGA SITOKI ILI USHINDE

HABARI KIMATAIFA

## Senegal kusitisha uhusiano wa kijeshi na Ufaransa

**DAKAR,** SENEGAL

TAMKO la Rais wa Senegal, Bassirou Diomaye Faye, kwamba hakutakuwa na wanajeshi wa Ufaransa nchini Senegal, limezidisha wasiwasi wa taifa hilo la Ulaya kupungua ushawishi wake kwa nchi za Afrika.

Hata hivyo, maswali yanasalia kuhusu ratiba na aina ya ushirikiano wa kijeshi wa siku zijazo kati ya nchi hizo mbili.

Rais Faye wakati akiongea na vyombo vya habari vya Ufaransa, alisema hivi karibuni hakutakuwa na wanajeshi wa nchi hiyo nchini Senegal.

Licha ya taarifa hiyo, hakuna ratiba ya uondoaji ambayo imetolewa na serikali ya Senegal.

Kumekuwepo kwa wimbi la nchi zilizotawaliwa na Ufaransa, kutangaza kusitisha uhusiano wa kijeshi kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo kutaka uhuru kamili wa kujitawala.

Chama tawala cha PASTEF kimekuwa kikitetea kuondolewa kwa kambi ya jeshi la Ufaransa nchini Senegal, kama kambi yoyote ya kigeni katika mpango wa kujitawala.

Kwa maana hiyo Rais Faye amethibitisha kikanuni wakati mipango mingine ikiendelea.

Mei mwaka jana, mara baada ya kuingia madarakani, Waziri Mkuu, Ousmane Sonko alieleza dhamira ya Senegal kutumia mamlaka yake, ambayo haiendani na uwepo wa kambi za kijeshi za kigeni katika ardhi yake.

Hata hivyo inatiliwa shaka sababu za mikataba ya ulinzi iliyosainiwa na nchi tatu.

Inabakia kuonekana jinsi zoezi hilo la kuondoa wanajeshi wa Ufaransa litafanya kazi.

Ufaransa tayari ilikuwa tayari imepanga kupunguza uwepo wa jeshi lake nchini Senegal kutoka askari 300 hadi 100 na kubadilisha kambi ya Dakar kuwa kambi ya wanajeshi wa Ufaransa na Senegal.

**RFI**

## Trump, Tradeau wakutana kujadili mvutano ulioibuka

**WASHINGTON,** MAREKANI

WAZIRI Mkuu wa Canada, Justin Trudeau, amekutana na Rais mteule wa Marekani, Donald Trump kufuatia tishio lake la kuiongezea nchi hiyo ushuru.

Trudeau alikutana juzi na Trump kwenye makazi yake binafsi ya Mar-a-Lago, yaliyoko Florida.

Mkutano huo unafanyika siku kadhaa baada ya Trump kusema ataiongezea Canada na Mexico asilimia 25 kodi kwa kuingiza bidhaa nchini Marekani, hadi mataifa hayo yatakapodhibiti uingizwaji wa dawa za kulevya na wahamiaji haramu wanaovuka mipaka na kuingia Marekani.

Tishio hilo la Trump limeibua mashaka nchini Canada, ambayo sehemu kubwa ya uchumi wake unaitegemea Marekani.

Wanauchumi wakikiri kwamba hatua kama hiyo itauathiri uchumi wa mataifa hayo mawili ambayo yanapakana na Marekani.

Trump amekuwa akiishutumu Canada kuwaruhusu wahamiaji kuvuka mpaka na kuingia Marekani kiasi ambacho katika uongozi wake wa awali alijenga ukuta katika mpaka wa nchi hizo mbili.

Hata hivyo, hakuna maelezo ya kina yaliyojadiliwa na viongozi hao wawili.

**DW**

# Waasi Syria wateka mji wa Aleppo

**DAMASCUS,** SYRIA

VIKOSI vya waasi nchini Syria vimedhibiti vitongoji kadhaa katika mji wa pili kwa ukubwa wa Aleppo.

Kwa mujibu wa shirika la uangalizi wa haki za bidamu la Syrian Observatory for Human Rights (SOHR) lenye makao yake nchini Uingereza, lilisema video kadhaa zinaonesha vikosi vya waasi vikiwa katika mji huo kama sehemu ya mashambulizi makubwa dhidi ya serikali.

Itakuwa mara ya kwanza kwa waasi wanaopigana na majeshi ya Rais Bashar al-Assad kufika Aleppo tangu walazimishwe kuondoka na jeshi 2016.

Vikosi vya waasi nchini Syria vimechukua udhibiti wa nusu ya mji huo.

Wakati huo huo, vikosi vya Russia vilianzisha mashambulizi ya anga katika sehemu za mji wa Aleppo usiku wa kuamkia jana katika kuwazuia waasi hao kusonga mbele.

Mashambulizi hayo makubwa yamefanyika kwa mara ya kwanza tangu 2016.

SOHR ilisema zaidi ya watu 300 ikiwa ni pamoja na raia 20 wameuawa tangu mashambulizi mapya kuanza Jumatano.

Mashambulizi hayo ni makubwa kufanywa dhidi ya serikali ya Syria kwa miaka mingi na ni mara ya kwanza kwa waasi wanaopigana na vikosi vya serikali kufika kwenye mji huo.

Safu ya makundi yenye silaha yanayoipinga serikali ya Assad ikiwa ni pamoja na wafuasi wa jihad, walichukua fursa ya ghasia na kunyakua maeneo mengi.

Serikali ya Syria kwa usaidizi wa Russia na washirika wengine, baadaye ilichukua tena maeneo mengi iliyokuwa imepoteza.

**BBC**



Waasi wa Syria wakiwa kwenye pikipiki katika barabara kuu ya kimataifa ya M5, kuelekea Aleppo. **PICHA: REUTERS**

# Korea Kaskazini yaapa kuisaidia Russia kijeshi

**PYONGYANG,** KOREA KASKAZINI

KIONGOZI wa Korea Kaskazini Kim Jong Un, amesema ataendelea kuisaidia Russia katika vita vyake dhidi ya Ukraine.

Kim ametoa hakikisho hilo mbele ya Waziri wa Ulinzi wa Russia, Andrei Belusov, ambaye ameanza ziara nchini humo.

Kim alinukuliwa na vyombo vya habari jana, akisema Korea Kaskazini itaunga mkono sera ya Russia ya kujilinda na kutetea uhuru wake dhidi ya hatua za kibabe za mabeberu.

Kim alikosoa hatua ya mataifa ya magharibi yakiongozwa na Marekani kwa kuiruhusu Ukraine kuyashambulia maeneo ya Russia kwa kutumia silaha zao za masafa marefu, na kuitaja kama uingiliaji wa moja kwa moja kwenye mzozo huo.

Alisema Russia inatumia haki yake ya kujilinda na kuhakikisha vikosi vya adui vinalipa gharama.

Katika hatua nyingine, Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky alisema nchi yake huenda ikakubaliana na Russia kusitisha mapigano ikiwa Jumuiya ya kujihami, NATO itatanua ulinzi wake nchini humo.

Rais Volodymyr Zelensky, alisema HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/ukraine-yatuma-vikosi-vipya-msitari-wa-mbele-zelenskiy-aomba-ulinzi-wa-nato/a-70925938" NATO inatakiwa kuutanua ulinzi wake hadi kwenye baadhi ya maeneo nchini humo ambayo bado yanadhibitiwa na Ukraine.

Alisema hayo katika mahojiano na kituo cha utangazaji cha Sky News cha nchini Uingereza.

Aliongeza kwamba wanatakiwa kufanya hivyo mara moja, kwani watatumia njia za kidiplomasia kuyarejesha maeneo yao yanayokaliwa na Russia.

Alisema, mpango huo haukuzingatiwa hapo awali kwa kuwa hakuna aliyependekeza rasmi.

**DW.**

# Vijana wapewa mbinu kukabiliana na uhaba ajira

**Na Grace Mwakalinga**

UHABA wa ajira na ukosefu wa maarifa muhimu ni changamoto kubwa inayowakabili vijana wengi nchini pamoja na kuwapo kwa fursa mbalimbali.

Vijana wengi hawajiandai ipasavyo kukidhi mahitaji ya soko la ajira, hali inayochangia kuongezeka kwa tatizo la ukosefu wa ajira.

Katika kukabiliana na changamoto hizo, Taasisi ya Her Initiative, kwa kushirikiana na Taasisi ya Sheria Kiganjani, inatekeleza Mradi wa Going Beyond wa miaka mitano unaolenga kuwapatia mafunzo maalum vijana namna ya kuchangamkia fursa za ajira na kujihusisha na ujasiriamali.

Mafunzo hayo, yalifanyika Dar es Salaam, yakiwanufaisha vijana 50 kupata ujuzi wa kujiajiri na kujiandaa kwa nafasi za ajira ndani na nje ya nchi.

Mwezeshaji Oswald Manyerere ambaye ni Mratibu wa Uhamasishaji Rasilimali, alisema vijana wengi wanakosa maarifa kwa sababu hawana njaa ya mafanikio.

Alisema wanatumia simu zao kufuatilia mambo yasiyowahusu katika mitandao ya kijamii, badala ya kutumia kupata taarifa zitakazowasaidia kuajiriwa na kujikwamua kiuchumi.

Gilian Mbaga kutoka Kazi Connect aliwataka vijana kutumia teknolojia kwa manufaa, kushiriki makongamano, na kutafuta fursa za kiuchumi kupitia njia bunifu.

Mkurugenzi wa Teknolojia wa Sheria Kiganjani, Musa Kisena, alisema kuna haja ya kuwasaidia vijana kuelewa wapi kuna fursa za ajira na jinsi ya kuziendea.

"Vijana wengi wanakutana na changamoto wakati wa kutafuta kazi, mara nyingi ni kwa sababu hawajui namna ya kuomba kazi au kujiandaa kwa usahihi, mafunzo haya yatawasaidia kuondokana na vikwazo hivyo," alisema Kisena.

Alisema mafunzo hayo ni sehemu ya utekelezaji wa Mradi wa Going Beyond, unaofadhiliwa na Digital Opportunity Trust (DOT) na MasterCard Foundation, ukilenga kuwasaidia vijana katika nchi za Tanzania, Malawi, Ivory Coast, na Zambia hadi mwaka 2028.

Kwa mujibu wa Ofisa Habari wa Her Initiative, Daniel Robert, mradi huo unatarajia kuwafikia vijana 1,500 ndani ya miezi sita ya kwanza.

Alisema wajasiriamali 300,000 kutoka nchi hizo nne, watanufaika na mafunzo hayo kwa kuimarisha biashara zao na kuongeza thamani ya bidhaa wanazozalisha.

"Tunalenga kuwasaidia vijana kujikwamua kiuchumi kupitia taaluma na biashara wanazofanya kwa kutumia njia bunifu na zenye ufanisi," alisema Robert.

Miongoni mwa vijana walionufaika na mafunzo hayo akiwamo, Isaya Richard, alisema amejifunza kuandika wasifu wa kitaalamu na barua za maombi ya kazi kwa kutumia mbinu zinazotakiwa.

Celine Julius alibainisha kuwa mafunzo hayo yamepokelewa vizuri zaidi na wanawake, ambao ushiriki wao umefikia asilimia 70, ukilinganisha na wanaume walioficha asilimia 30.



Mjasiriamali akiwa amebeba bidhaa zake akitafuta wateja barabara ya Mwenge Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Viongozi wapya serikali za mitaa wafundwa

**Na Steven William** MUHEZA

WENYEVITI wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji na wajumbe ambao wamechaguliwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa uliofanyika Novemba 27, mwaka huu, wametakiwa kuwatumikia wananchi.

Pia wametakiwa kujenga nidhamu, weledi, kujituma na kuwasaidia wananchi kutatua kero zinazowakabili.

Wito huo ulitolewa juzi na Mwenyekiti wa Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi nchini na mbunge mstaafu wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu.

Alisema wananchi wamewachagua viongozi hao ili wawasaidie kuwatatulia matatizo yao na kuwaletea maendeleo katika wilaya ya Muheza na taifa kwa ujumla.

Balozi Adadi aliwaomba wateule hao kufanya kazi kwa bidii za kuleta maendeleo ili kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan ambae kwa sasa ameleta maendeleo makubwa katika miradi mbalimbali nchini.

Alisema anaamini viongozi hao watafanya kazi kwa nidhamu, weledi na kufuata taratibu na sheria ya nchi pamoja na kutatua migogoro mbalimbali maeneo yao.

Mmoja wa wananchi walioshiriki katika uchaguzi huo, Juma Meta, alisema uchaguzi wa serikali za mitaa ni moja ya sehemu za kujipanga katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2025 wa kuchagua Rais, Wabunge na Madiwani.

Wakazi wengine wa mtaa wa Majengo wilayani hapa, Mauld Meta, Azizi Adadi na Abdul Ayoub, kwa nyakati tofauti walisema walikwenda kupigakura kuwachagua viongozi hao kwa kuwa kukosa kufanya hivyo ni kupoteza haki zao.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Huyu ndiye Chakubanga aliyejiita John Smith



**Na Adam Fungamwango**

UNAWEZA ukadhani ulikuwa utunzi wa kufikirika. Huu ni utunzi wa kisa cha kweli kabisa ambacho kilitokea kwenye miaka ya 1980.

Kila kilichoimbwa kwenye wimbo huu na Marijani Rajabu ni cha kweli kabisa na alimtungia mmoja wa ndugu zake wa karibu. Mashabiki waliupa majina mbalimbali kama 'Awe Mwana', 'Chakubanga', 'Mwana Vibaya', lakini jina lake halisi ni 'Mwana Acha Ujinga'.

Haya mambo ya baadhi ya vijana kwenda nchi za nje, wakirejea wanakuwa wamebadilika hata tabia zao yalianza zamani sana. Iwe walioenda kwa ajili ya masomo, au kwa kazi ya ubaharia, mara nyingi waliporejea nchini walikuwa na mambo mengi, mbwembwe na vituko vingi vilivyowashangaza wengi.

Wimbo huu wa Marijani ni uthibitisho wa baadhi ya vituko na tabia za baadhi ya vijana wa wakati huo baada ya kurejea kutoka Ulaya, watoto wa mjini zamani walikuita 'ng'ambo'.

"Leo kijana ninasema eee, hayo mambo yako unayofanya eee, mwisho wake mwana mambo yanakuwa mabaya, wala usidanganyike na cheo ulichopata, kudharau wazazi kuhadaika na dunia, mwana vibaya, vibaya mwana vibaya aaa.

Fikiri kwanza ulikotoka eee, usijifanye huna baba wala mama, waliokulea kwa tabu nyingi na mashaka, waliokusomesha bwana ukahitimu mafunzo, mbona unawanyanyasa na matusi kuwatukana, mwana vibaya ee, vibaya mwana vibaya aaa."

Huyu jamaa pamoja na kwamba baba na mama yake waliuza ufuta na karanga kwa ajili ya kumsomesha ili aje kuwasaidia baadaye, lakini imegeuka. Amekuwa akiwadharau na kuwatukana, kisa hawajasoma, na masikini.

"Mambo ya ajabu uliyofanya, ulipochaguliwa kwenda mambo, uliporudi bwana na jina umebadilisha, jina lako chakubanga, ukajiita John Smith na mwendo umebadili bega moja umelishusha, mwana vibaye ee, vibaya mwana vibaya aaa.

Mpaka sasa nyumbani hufiki, umefikia kwa marafiki, ati unasema kuna vumbi jingi sana, wala hukumbuki baba, humo ndimo ulimozaliwa, ugali na kisamvu ndicho kilichokukuza, mwana vibaya ee, vibaya mwana vibaya aaa.

"Utembeaji wa kushusha bega moja ulikuwa maarufu sana zamani kwa vijana watoto wa mjini, hasa wale mabaharia, waliozamia meli wakati huo na kufanikiwa kurejea nchini wakiwa wamefanikiwa kupata maisha mazuri, wakati huo wakiita 'wameukata'.

Jamaa kaenda Ulaya, aliporudi kila kitu kimebadilika, amebadilisha jina na mwendo, hataki kurudi kwao kwa sababu ni duni. Msomi kama yeye hawezi kukaa kwenye kibanda 'mbavu za mbwa'. Badala yake amefikia kwa marafiki, wengine walikuwa wanafikia hotelini.

"Mama yako kakutafuta eee, mzee wa watu kahangaika ee, kakusaka mama kwa bahati kakuona, ulipomuona mama, ukajifanya humjui mama, unawauliza marafiki, wamuulize ana shida gani, anajibu chakubanga, unamwambia hapa hayupo, wewe siyo chakubanga, ila wewe ni John Smith, mama kaondo, analia mama analia, anaona uchungu, analia mama analia aaa."

Damu nzito kuliko maji, mama baada ya kusikia kijana wake amerejea kutoka Ulaya na amefikia kwa rafiki zake, akamtafuta mpaka akamuona.

Jamaa alipomwona akajifanya hamjui, akawauliza marafiki zake, bi mkubwa amefuata nini hapa? Mama anajibu nimemfuata mwanangu Chakubanga, jamaa anawaambia wenzake, mwambieni hakuna mtu kama huyo hapa. Mama anashangaa na kuuliza wewe siyo Chakubanga? Kijana anamwambia hajawahi kuitwa Chakubanga, yeye ametoka ng'ambo bwana anaitwa John Smith. Baada ya tukio hilo mama anaondoka huku akilia kwa uchungu. Hebu fikiria, baada ya tukio hilo nini kitafuata?

Kama nilivyosema hicho kilikuwa kisa cha kweli cha mmoja wa ndugu wa Marijani, akakitungia wimbo kudhihirisha kuwa wanamuziki wa zamani walikuwa mahiri kwa kutunga matukio mengi ya kweli, yaliyo ndani ya jamii na yataendelea kutokea kwenye uso wa dunia. Na ndiyo maana nyimbo zao hazichuji.

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-11

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NDIYO mimi naishi na mwanamke ambaye nataka kumuoa, ingawa hakai mara kwa mara kutokana na kuwa ana kazi, hivyo mtoto muda mrefu anakuwa na hausigeli." "Nitakuuliza swali la mwisho." "Uliza tu bwana mwandishi." "Mligombana nini, au mliachana vipi?" Mimi binafsi sijui. Ila nilianza kuona vituko tu. Vituko vilianza kila siku kituko baada ya kituko, siku ya siku narudi kazini nakuta amebeba kila kitu ndani. Ilibidi nimsake, mara nikaambiwa kaenda kwa dada yake, mara wapi, kwao hakurudi. Ilibidi nianze maisha upya kwa tabu. Talaka nilimpa baadaye baada ya usuluhishi kushindikana."

Eddy aliridhika na majibu ya Macky. Akaangalia muda wake. ilikuwa imetimu saa 9:00 alasiri.

"Nikurudishe na gari yangu, au nikupe pesa za kukodi mwenyewe usafiri?" Akauliza. "Nitashukuru kama ukinipa pesa, maana hapa itakayobaki inaweza kunisaidia."

Bado hakukuwa na mwanga wowote, kwani maswali mengi aliyomuuliza yalionekana ni ya kifamilia zaidi na si ya kikazi. Yale ambayo alipaswa amuulize ili kupigisha hatua kuelekea kuwapata wahusika.

Alichopanga sasa Eddy, kesho yake ni kumpata Dora, mama mzazi wa Macaire ili naye ampe chochote ambacho kinaweza kumsaidia kwenye upelelezi wake. Ikiwezekana na yeye ajibu maswali ya kifamilia kama aliyoyajibu Macky. Alivutiwa tu kutaka kujua nani anaweza kuwa mkweli na nani muongo kuhusu kuachana kwao. Alijua kila mmoja atavutia kwake. Lakini yeye kama mpelelezi atafahamu nani anayezungumza kweli kati yao.

"Umepata meseji yoyote kwa watekaji?" Ndiyo. "Lini?" Jana usiku. "Safari hii wamesema ukaweke pesa wapi?" Mh! Bwana mwandishi huko unakokwenda mbali sasa. Kumbuka mtoto wangu mpaka sasa hapatikani kwa sababu kuna watu wanatoa taarifa sasa na wewe nikikwambia, si ndio yatakuwa yale yale, maana tutaongeza tena utata." Eddy alivutiwa na jibu lake. Ni kweli kabisa yeye amejitambulisha kama mwandishi, hivyo anapaswa kuuliza maswali ambayo alipaswa kuuliza na sio yanayoingia moja kwa moja upelelezi, ikiwamo kujua wapi pesa zitapelekwa kuwekwa kwa amri ya watekaji.

"Sikiliza nikwambie Macky. Kuna kitu nataka kukusaidia kuhusu hili!"




**"Usihofu, nina rafiki yangu ana uwezo mkubwa wa kifedha. Anaweza kutuaidia ili kuondokana na adha ya kuwaambia askari polisi kiasi mpaka baadhi yao ambao si waaminifu wanavujisha siri." Macky alionekana kufikiria kuhusu hilo, halafu akauliza. "**

Macky alionyesha mshangao. Wakati huo walikuwa wamesimama kutaka kuondoka, lakini ni kama mazungumzo yalianza upya.

"Mimi nataka kukusaidia kukupa Sh. Milioni 15 kwa kuwapa watekaji." Macky akazidi kupata mshangao na kushindwa kusema chochote. "Usihofu, nina rafiki yangu ana uwezo mkubwa wa kifedha. Anaweza kutuaidia ili kuondokana na adha ya kuwaambia askari polisi kiasi mpaka baadhi yao ambao si waaminifu wanavujisha siri." Macky alionekana kufikiria kuhusu hilo, halafu akauliza. "Ni za mtego au mkopo?" Una maana gani? Eddy akauliza.

"Unajua Jeshi la Polisi ndilo mara zote linatoa hizo pesa. Linatoa kwenye mfuko wake na lengo sio kuwapa ila mtego. Yaani nia ni kuwakamata, sio kuwapa hizo pesa na mtoto kuachiwa. Sasa hizo unazotaka kutoa ni za namna gani? Maana kama ni za mkopo haiwezekani, maana siwezi kujua baada ya hapo, mimi na ndugu zangu tunachukua muda gani hadi kuzichanga mpaka kufikia kiasi hicho."

"Zitakuwa za mkopo! Rafiki yangu huyo hana tatizo! Hukopesha pesa kiasi cha Sh. Milioni 15 na kurejesha kidogo kidogo kwa mwaka mzima. Kama ndugu mtajipanga mnaweza kurudisha kabla hata mwaka. Ila mimi binafsi kabla ya kukuletea hizo pesa nina ushauri." "Enhee niambie." "Pesa zikishafika, hakuna kumwambia mzazi mwenzio wala askari polisi. Iwe siri na mimi na wewe. Tuwapelekee tu wachukue watuachie mtoto, halafu kulipa iwe taratibu hadi mnamaliza." "Mhh! Mbona naona kama naanza kukuelewa hivi?" "Lazima utanielewa tu mtu wangu." "Unajua hata mimi sijui hawa jamaa wanajuaje. Sasa kama wanajua safari hii wajue kuwa pesa hazitoki tena polisi na wala hawawindwi kukamatwa, hapa nadhani sasa mtoto tutampata." "Swadakta hilo ndilo wazo langu." Macky alimkumbatia Eddy. Machozi yakamtoka. "Ukifanikisha hili, mwandishi utakuwa sio rafiki yangu tu, bali ni ndugu yangu wa damu." "Onyo, usimwambie mzazi mwenzio wala askari yeyote." Eddy akazidi kusisitiza. "Yaani nimeanza kukuamini sasa. Kwa maana hiyo nitakwambia yote waliyoniambia.

Pesa za safari hii wamesema nipeleke Kigamboni, keshokutwa, katikati ya msitu mdogo utokao Kibada kwenda Tuangoma. Upande wa kulia kama unakwenda Tuangoma kuna ujenzi wa kiwanda unaoendelea. Mwisho wa uzio wa kiwanda hicho kwa mbele, ndipo pesa hizo zinatakiwa kuwekwa.

Na wamesema iwe saa nne usiku kwa sababu ni msitu hivi." "Na mtoto utampataje?" "Wameniambia kama dili ikifanikiwa, mtoto watamuachia kesho yake asubuhi na wao ndio watanipigia simu niende sehemu ambayo watamuacha, na itakuwa ni sehemu salama."

*******************************

"Unaitwa nani?" "Dora Mathias." "Pole sana kwa tukio hili la mtoto wako kutekwa." Ahsante sana bwana mwandishi." "Kabla ya tukio hili naomba nikurudishe nyuma kidogo. Ni kitu gani kilisababisha wewe na Macky mkatengana?" "Kaka yangu we, unajua wakati mwingine nyinyi wanaume mna matatizo. Mwanume huyu nilikuwa sijui nguo yake, kula ya shida, kila kitu matatizo, nikaona cha kufia nini, nikajiondokea."

Eddy hakutaka kumwambia chochote kile juu ya Macky. Hakutaka Dora atambue kama ameshakutana na Macky kwani angeanza kuwa na wasiwasi kuwa huenda wameongea mengi, ya ukweli na ya uongo.

"Sasa unasikia dada yangu, achana na hao askari, maana inaonekana kuna mtu anatoa anawapa taarifa, mimi nataka kukusaidia mtoto wako aachiwe huru. Nataka nikusaidie kiasi cha Sh. Milioni 15 ambazo nitazikopa kutoka kwa rafiki yangu." Macho yalimtoka pima Dora na kumuuliza Eddy,"unasema kweli?" "Ni kweli kabisa." "Mbona nitashukuru maana nina hamu na mwanangu ndugu mwandishi."

Ilikuwa ni siku ya pili baada ya Eddy kuongea na baba wa mtoto aliyetekwa, na sasa alikuwa anaongea na mama yake mzazi. Ikumbukwe wote wawili walingea kwa nyakati tofauti na Eddy, bila kujua kuwa ni mpelelezi anayetaka kuwakamata waliomteka mtoto wao, lakini kujua ni kitu gani kinakwamisha wahusika watiwe mbaroni kwani wanaonekana wanajua kila kinachofanyika kutoka kwa maafande na wazazi.

"Hizi ni mimi mwenyewe nimeamua kukupa, nitazilipa mwenyewe taratibu. Ninachotaka kufanya ni kwamba tukaweke sehemu ambayo wataamua ili mtoto wako apatikane arudi nyumbani. na Hili hatuishirikisha polisi. Ni kwamba nataka watekaji wachukue pesa ili wamuachie mtoto na si mtego kama wanavyofanya polisi." Dora alionekana kupatwa mshagao asiamini anachokisikia. "Unasema kweli?" "Kweli bibie!" "Mbona nitashukuru sana jamani, mtoto wangu sijamuona siku nyingi." Alisema na kuanza kulia. Eddy alipata kazi ya dakika kama tano hivi ya kumbembeleza.

Alipokaa sawa akamuuliza. "Enhe sasa tutajuaje kama watekaji hao ni lini watautaka mzigo huo kwa sababu anayepigiwa siku zote na kuamrishwa ni mzazi mwenzako tu?" Lilionekana ni swali muhimu mno kwa Dora.

**Itaendelea Jumapili**



# DAVIDO ALIANZA MUZIKI KWA SIRI

MWANAMUZIKI maarufu wa Afro Beats kutoka Nigeria, Davido, ameibua mjadala baada ya kueleza kuwa wakati akiwa katika harakati za kuingia muziki, baba yake alikuwa hajui chochote.

Amesema hata alipoanzisha studio ndani ya nyumba yao, baba yake hakufahamu chochote zaidi ya ndugu zake wa karibu.

Davido amesema nyumba yao ilikuwa ina vyumba zaidi ya 20 na haikuwa rahisi baba yake kujua kama ana Studio, licha ya kupishana na watu walikuwa wanangia kurekodi.

"Nilikuwa na studio ndani ya nyumba na hakujua, nyumba ni kubwa sana ina vyumba kama ishirini na kitu".

Davido anasema aliamua kufanya hivyo sababu ya mapenzi yake makubwa kwenye muziki kuliko hata ilivyokuwa kwenye elimu.

# Ukimtaka Phina ujipange

STAA wa muziki wa Bongo Fleva, Phina, amesema mwanaume anayetaka kumuoa lazima atambue kwamba yeye ni mvivu wa kufua nguo kwa kutumia mikono.

Akizungumza na EATV, Phina amesema sio kwamba hawezi kufua, lakini hapendi kuinamisha mgongo kwake ni jambo gumu na linampa shida.

"Kuinamisha mgongo ndugu yangu kwa kweli ni ngumu, hasa ukikutana na majeans ," amesema Phina.



## ZISIKUPITE

### ARNOLD ANUKIA MADRID

REAL Madrid wameifahamisha Liverpool kuhusu nia yao ya kutaka kumsajili beki wa England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26. ***(TalkSport)***

### AMORIM KUTOSAJILI JANUARI

KOCHA mpya wa Manchester United, Ruben Amorim ameazimia kufanya kazi na wachezaji wake wa sasa na hajatuma ombi kwa uongozi wa klabu kuhusu usajili wowote wa Januari. ***(Sky Sports)***

### GEERTRUIDA AWANIWA SPURS

KLABU ya Tottenham Hotspur ina nia ya kumsajili beki wa kulia wa RB Leipzig, Lutsharel Geertruida mweney umri wa miaka 24, kama kiungo mbadala wa Pedro Porro, mwenye umri wa miaka 25, ambaye analengwa na Real Madrid . ***(Caught Offside)***

### DELAP AVUTIA

MSHAMBULIAJI wa Ipswich Town mwenye umri wa miaka 21, Liam Delap anavutiwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England. ***(Athletic)***

### CUNHA AHUSISHWA NA MAN

KLABU ya Manchester United na Tottenham Hotspur zinaendelea kuhusishwa na taarifa za kutaka kumnunua Cunha, lakini kocha wa Wolves, Gary O'Neil amekataa kumruhusu kuondoka Januari. ***(MEN)***

### SCHMID HUYO VILLA

KLABU ya Aston Villa inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili kiungo wa kati wa Werner Bremen na Austria, Romano Schmid mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

### DORGU AWINDWA CHELSEA

CHELSEA inaongoza katika mbio za kumsajili beki wa Denmark, Patrick Dorgu mwenye umri wa miaka 20 kutoka Lecce, ambaye anaweza kuhitaji malipo ya takribani pauni milioni 50. ***(Caught Offside)***

### CALVERT-LEWIN KUBAKISHWA

EVERTON inataka kuendelea kuwa na mshambuliaji wa England, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27 Januari, licha ya uvumi kuhusu mustakabali wake. ***(Football Insider)***

### GYOKERES HAITAKI ARSENAL

HATUA ya Arsenal ya kutaka mshambuliaji mpya imepata pigo kwani Viktor Gyokeres mwenye umri wa miaka 26 wanayemtaka, anataka kumfuata kocha wake wa zamani wa Sporting Lisbon, Ruben Amorim kule Manchester United. ***(Football.London)***

### ATAKA KURUDI CHELSEA

MLINZI wa Crystal Palace mwenye umri wa miaka 24, Marc Guehi anatamani kujiunga tena na Chelsea, wakati Newcastle United pia bado inavutiwa na beki huyo wa kati. ***(TeamTalks***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# SANCHO APEWA MTIHANI CHELSEA

**LONDON,** England

### Kocha wake amtaka awe fiti kimwili na kiakili ili apate nafasi kwenye...

ENZO Maresca amempa mtihani Jadon Sancho kwamba ni lazima awe fiti kiakili na kimwili kama anataka kurejesha nafasi yake kwenye kikosi cha kwanza cha Chelsea.

**Sancho alianza vyema soka lake pale Chelsea, kwa kutoa pasi za mabao katika mechi tatu mfululizo baada ya uhamisho wake wa mkopo kutoka Manchester United, lakini aliondolewa kwa sababu za kimkakati katikati ya kipindi cha kipigo kutoka kwa Liverpool mnamo Oktoba 20 na baadaye akawa nje ya uwanja kutokana na jeraha.**

Winga huyo alirejea akitokea benchi kama mchezaji wa akiba katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Leicester City na kisha akapiga pasi mbili za mabao katika ushindi wa Ligi ya Europa Conference dhidi ya Heidenheim, ambapo Maresca alimpa Sancho njia ya kurejea kwenye kikosi cha kwanza katika Ligi Kuu England.

"Nilisema tangu mwanzo, Jadon ni muhimu sana kwetu," alisema Maresca.

"Ni muhimu sana. Anatakiwa kuwa fiti kiakili na kimwili, atatusaidia sana. Kwa bahati mbaya hatukumtumia katika michezo michache iliyopita lakini anaonesha sasa jinsi alivyo muhimu kwetu.

"Hasa dhidi ya timu zinazolinda safu ya chini, tunahitaji ubora huo katika tatu ya mwisho. Wakati mwingine atapiga zaidi lakini nadhani atatusaidia sana."

Mambo yanayotatiza kwa Sancho ni uwepo wa wachezaji wengi mbadala katika nafasi yake.

Noni Madueke amekuwa akianza kikosi cha kwanza, wakati mchezaji mwingine aliyesajiliwa majira ya joto, Pedro Neto amejipatia dakika zaidi, huku Mykhailo Mudryk pia ameongeza kesi ya kiwango chake.

"Tunahitaji wote wachukue nafasi wanapozipata," aliongeza Maresca kuhusu kikosi cha Chelsea.

"Tuna wachezaji 24 au 25 na ni wazuri ambao wote wanastahili kucheza na wanafanya kazi ya kustaajabisha. Tutashiriki dakika katika michezo inayofuata kwa sababu tuna michezo mingi kwa hiyo ni jambo la kawaida wao kujituma."

# KONATE: NITAKUWA NJE KWA KIPINDI KIREFU




**LIVERPOOL,** England

MLINZI wa Liverpool, Ibrahima Konate amethibitisha kuwa anakabiliwa na kipindi kirefu cha kukaa nje ya uwanja baada ya kuumia kwenye ushindi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Real Madrid Jumatano.

Mfaransa huyo aliwasaidia Wekundu hao kwa pasi yake nzuri dhidi ya Kylian Mbappe na Jude Bellingham.

Konate ameanza mechi 11 kati ya 12 za Ligi Kuu za Liverpool hadi sasa, aliingia kama mchezaji wa akiba wakati wa ushindi wa wikendi ya ufunguzi dhidi ya Ipswich Town mnamo Agosti, lakini sasa amefichua kuwa anaanza kujiuguza baada ya kusaidiwa kutoka uwanjani alipogongana na Endrick wa Madrid.

Alichapisha kwenye Instagram: "Inasikitisha sana kupata jeraha hili mwishoni mwa mchezo mzuri Jumatano usiku.

"Sasa tunaanza mchakato wa kupona lakini jambo moja ninaloahidi nitarudi na kuwa bora zaidi.

"Asante kwa sapoti ya ajabu pale Anfield. Inshallah tutaendelea na nitaisapoti timu kila hatua."

Liverpool wanaweza kuendeleza faida yao dhidi ya City wakiwa kileleni mwa jedwali kwa ushindi wa Anfield lakini kocha, Arne Slot sasa ana kitendawili cha kikosi cha kwanza huku Konate akiwa hayupo.

# Barca kumuuza de Jong



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA itajaribu kumtoa Frenkie de Jong na kuondoa mshahara wake mkubwa msimu wa joto unaokuja baada ya kuvunjika kwa mazungumzo ya mkataba mpya, kwa mujibu wa ripoti nchini Hispania.

Kiungo huyo wa kati wa Uholanzi amekuwa akiandamwa na majeraha katika miaka ya hivi karibuni.

Wakati wa zaidi ya miezi mitano akiwa kando na tatizo kubwa la kifundo cha mguu, De Jong alihofia kuwa muda wake unaweza kumalizika.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 amekuwa akitumiwa kwa kiasi kidogo na Hansi Flick msimu huu, na huenda akaingia katika miezi yake ya mwisho pale Katalunya ikiwa Barcelona itashindwa kumpatia mkataba mpya.

De Jong ana mkataba ambao utamalizika mwaka 2026, lakini mazungumzo juu ya uwezekano wa kuongezwa - ambayo yatahusisha marekebisho makubwa ya mshahara.

Miamba hao wa Katalunya kwa sasa wamejikita katika kumuuza kiungo huyo wa kati wa gharama kubwa wakati wa dirisha la kiangazi, kwa mujibu wa Sport.

Barcelona wanasemekana kuwa tayari kupunguza ada ya uhamisho, wakati wa kuzingatia awamu za ada ya uhamisho ya De Jong, kwani mchezaji huyo anagharimu kiasi cha euro milioni 35 kwa mwaka.

Inasemekana viongozi hao wa sasa wa LaLiga walimpa De Jong hati ya mwisho mwezi Oktoba, wakimtaka asaini mkataba mpya kabla ya dirisha la uhamisho la Januari ikiwa anataka kusalia katika klabu hiyo.

Manchester United walikuwa wamuwania kwa muda mrefu huku Erik ten Hag - kocha wa zamani wa Ajax De Jong - akiwa Old Trafford.

Chelsea na Paris Saint-Germain pia wamekuwa wakihusishwa na kiungo huyo wa kati, huku Liverpool nao wanamhitaji.

Mkurugenzi wa michezo wa Barcelona, Deco alifuta mazungumzo ya uwezekano wa kuondoka kwa De Jong mnamo Septemba, akisisitiza: "Ana mkataba na Barca na tunafurahi naye."

# Arsenal kutosajili Januari

**LONDON,** England

ARSENAL itatafuta kuimarisha kikosi cha Mikel Arteta mnamo 2025 lakini hakuna uwezekano wa kufanya usajili Januari, ripoti zimefichua.

Mgogoro wa majeraha ulichangia kuanza kwa msimu kwa kusuasua kwa Arsenal, na wamerudi kwenye kiwango katika wiki za karibuni, lakini bado wanajikuta wakishuka katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu, pointi tisa nyuma ya vinara Liverpool.

Arsenal haijawahi kuogopa kuingia katika soko la usajili Januari, kwani waliwasajili Jorginho na Leandro Trossard, lakini ESPN imesema hakuna uwezekano wa kuwa na uhamisho wowote wakati huu.

Hakika, Arsenal wasipojikuta wakikabiliwa na tatizo lingine la jeraha, hawatarajiwi kukiongezea nguvu kikosi Januari na badala yake wataendelea na maandalizi ya kile ambacho kinaweza kuwa muhimu kiangazi.

The Athletic limeongeza kuwa kuna mipango ya wachezaji kadhaa wa kuwasajili, ikiwa ni pamoja na mshambuliaji mpya na winga ambaye atasaidiana na Bukayo Saka.

Viktor Gyokeres wa Sporting CP na mwenzake wa Sweden, Alexander Isak wa Newcastle United wote ni miongoni mwa walengwa wa Arsenal.

Gyokeres anaweza kupatikana kwa karibu euro milioni 70, wakati Isak anatarajiwa kugharimu karibu mara mbili ya kiasi hicho.

Wakati huohuo, Arsenal wanataka kuongeza safu yao ya kiungo na vijana zaidi huku wakijiandaa kwa kuondoka kwa Jorginho na Thomas Partey.

Mchezaji aliyesajiliwa majira ya joto, Mikel Merino ana umri wa miaka 28 na haisaidii kupunguza wastani wa umri wa kikosi.

Arsenal pia itatafuta kusajili angalau golikipa mmoja mpya ili kushindana na David Raya.



HABARI MICHEZO

## Yanga, Simba zakwepana

INATOKA UK. 24

Alisema kuwa kiongozi huyo alipigwa na mawimbi makali, lakini alisimama imara na kufanya maboresho ndani ya klabu na timu akishirikiana na wenzake, hatimaye leo wanachama na mashabiki wameanza kula mema.

"Mafanikio yaliyoanza kuchomoza sasa ndani ya klabu yetu ni kutokana na uimara wa viongozi wetu wa klabu wakiongozwa na Mwenyekiti wetu Murtaza Mangungu.

Mawimbi makali yalimpiga Mwenyekiti wetu lakini alisimama thabiti na kufanya maboresho ndani ya klabu yetu akishirikiana na viongozi wenzie na hatimaye leo tumeanza kula mema ya Simba

Jukumu letu wana Simba ni kuwaombea viongozi wetu waendelee kuwa madhubuti kwa maslahi ya klabu yetu," alisema Ahmed.

## Azam yapania kileleni leo

INATOKA UK. 24

mzuri," alisema Thabit, maarufu kama Zaka Zakazi.

Tangu ilipolazimishwa suluhu dhidi ya Mashujaa FC, Septemba 29 mwaka huu, Uwanja wa Lake Tanganyika Kigoma, Azam ilianza kupata ushindi mfululizo hadi kufikia michezo sita kwa kuifunga Namungo bao 1-0, ikaishindilia Prisons mabao 2-0, ikaipa kipigo cha mabao 4-1, KenGold, kabla ya kuichapa Yanga bao 1-0, baada ya hapo ikaifunga Kagera Sugar bao 1-0, kabla ya juzi kushinda mabao 2-1, mechi ikichezwa, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Dodoma, Moses Mpunga amesema wamejiandaa vyema na mchezo huo, ikiwemo kuipa kipigo Azam FC ili kutuma ujumbe kwa timu zingine kuwa Uwanja wa Jamhuri ni machinjioni.

"Katika mechi hii tunataka kutuma ujumbe kuwa Uwanja wa Jamhuri Dodoma si sehemu salama kwa timu za Ligi Kuu zikija hapa, huu ni uwanja mgumu, kila mmoja anauogopa, ni machinjioni hapa, tumejiandaa vizuri," alisema Mpunga.

Dodoma Jiji imeshinda mechi zake nne kwenye uwanja huo, kati ya tano ilizocheza, ambapo imepoteza mechi moja tu dhidi ya Simba ikifungwa bao 1-0, mechi iliyochezwa, Septemba 29, mwaka huu.

Wakati Azam ikiingia uwanjani leo ikiwa kwenye nafasi ya pili kwa michezo 12 iliyocheza, Dodoma Jiji ipo nafasi ya tisa, ikiwa imeshacheza mechi 12, ikikusanya pointi 16.

# TABORA YAAHIDIWA MILIONI 200 IKIMALIZA TATU BORA

**Na Adam Fungamwango**

MKUU wa mkoa wa Tabora, Paul Chacha, ameipongeza timu ya Tabora United kwa kuendelea kufanya vyema kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara, huku akiahidi kuizawadia Sh. Milioni 200 iwapo itamaliza kwenye nafasi tatu za juu.

**Mkuu wa mkoa huyo alisema hayo mkoani humo baada ya timu hiyo kuifunga KMC mabao 2-0, mechi iliyochezwa juzi Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam, ikiwa ni mechi ya tano kwa timu hiyo kucheza bila kupoteza.**

"Wao wanatakiwa wajitahidi tu, wakimaliza kwenye nafasi tatu za juu ligi itakapokuwa imeisha, yaani ligi imeisha na wapo ndani ya tatu bora, tunawawekea Sh. Milioni 2000 mezani, zawadi yao hiyo. Wakishindwa sasa hiyo ni juu yao, lakini sisi tumeamua hivyo, ile ni timu yetu ya mkoa tunatakiwa kuilea. Walikuwa hawana basi tumewanunulia, kwa sasa hawana shida na mishahara wala posho yoyote kila kitu kiko sawa, wakishindwa kucheza mpira ni wao," alisema Mkuu wa mkoa huyo.



Aliwapongeza wachezaji, benchi la ufundi na viongozi kwa kuendelea kuutangaza vyema mkoa huo, akiahidi kuwa nao bega kwa bega kwa kila mahitaji yatakayohitajika.

Ushindi wa juzi umeifanya timu hiyo kucheza michezo mitano bila kupoteza, ambapo mara ya mwisho ilichapwa mabao 4-2 na JKT Tanzania kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, Oktoba 18 mwaka huu.

Baada ya hapo ilimtimua kocha, Francis Kimanzi na ikaanza kwa kushinda wa bao 1-0 dhidi ya Pamba Jiji, bao 1-0 dhidi ya Mashujaa FC, ikaitandika Yanga mabao 3-1, ikatoka sare ya bao 2-2 na Singida Black Stars, kabla ya juzi kuitandika KMC nyumbani kwao mabao 2-0.

Ushindi huo umeipeleka Tabora United hadi nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikifikisha pointi 21 katika michezo 13 iliyocheza, ikishinda mechi sita, sare tatu na kupoteza nne.

Kipigo hicho imeifanya KMC kushuka hadi nafasi ya 10 ya msimamo, ikisalia na pointi 14, ikicheza michezo 13, ikishinda nne, sare mbili na kupoteza michezo saba.



Msemaji wa zamani wa klabu ya Yanga, Haji Manara (kushoto) ambaye kwa sasa ni msemaji wa kampeni ya Magift akimpongeza mshindi magifti ya kujift, Asia Mlay (katikati) ambaye ni mwanafunzi wa Chuo baada ya kutangazwa mshindi. Kulia ni Ofisa Mkuu wa Mixx by Yas, Angelica Pesha. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Inter Zanzibar kujipanga mzunguko wa pili*

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

KOCHA wa Inter Zanzibar FC, Hassan Mohmed amesema licha ya kupokea vipigo mfululizo katika michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar, lakini bado anaimani timu hiyo itafanya vizuri katika mzunguko wa lala salama.

Inter Zanzibar imeendelea kugawa alama katika michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar inayoendelea Visiwani hapa, ambapo juzi Ijumaa katika michezo wao wa 14 ilifungwa mabao 4-1 na Mwenge SC kutokea Pemba.

Akizungumza mara baada ya mchezo huo, kocha Mohamed alisema bado wana nafasi ya kurekebisha makosa yao na kurudi tena upya kwa kufanya mipango itakayo kuwa na faida ili kupata alama za kuwabakisha Ligi kuu.

Alisema bado ni mapema kupoteza matumaini ya kubaki ligi kuu kwakuwa mipango yao ni kuhakikisha wanakifanyia maboresho makubwa kikosi chao.

"Bado tunayo nafasi ya kuibakisha timu ligi kuu kwa kujipanga upya, mzunguko wa kwanza hatukuwa vizuri," alisema.

Inter Zanzibar sasa imefungwa michezo 11 kati ya 14 iliyocheza na imemeshinda mchezo mmoja na kutoka sare mara mbili.

Na sasa ipo nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na alama tano, wakati anayeburuza mkia ni Tekeleza FC yenye alama tatu.

# Michezo

Jumapili Desemba 1, 2024
Nipashe



Arsenal kutosajili Januari UKURASA 22



Kocha wa Simba Davies Fadlu



Kocha wa Yanga Saed Ramovic

# YANGA NA SIMBA SC ZAKWEPANA ALGERIA

**Na Adam Fungamwango**

Tetesi zilidai zitatumia usafiri mmoja kwenda nchini humo, lakini zote zime...

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye mechi za kimataifa, Yanga na Simba zimeonekana kukwepana kwenda pamoja nchini Algeria kwa kutumia ndege moja, baada ya kila mmoja kupanga tarehe tofauti.

Habari zilizopatikana kutoka ndani ya klabu hizo mbili zinasema kuwa kila timu ina itifaki zake, hivyo Yanga imepanga kuondoka Jumanne ijayo, huku Simba ikipanga kuondoka Jumatano zote zikienda nchini Algeria kucheza mechi za kimataifa kwenye miji tofauti.

Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga, inatarajiwa kuondoka Jumanne ijayo na itafikia kwenye mji wa Algiers kucheza mechi ya pili ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya MC Alger, itakayopigwa Jumamosi ijayo saa 4:00 usiku, Uwanja wa Julliet wa Tano.

**“Sisi Mungu akipenda tutaondoka Jumanne kwenda Algeria kwa ajili ya mchezo huo, hatujapanga na mtu, huu ni utaratibu ambao tumeuweka sisi wenyewe,” alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu ya Yanga.**

Simba yenyewe inatarajia kwenda kucheza mchezo wa pili wa makundi wa Kombe la Shirikisho katika Kundi A dhidi ya CS Constantine na inatarajiwa kuondoka nchini Jumatano na kufikia kwenye mji wa Constantine ambako ndiko makao makuu ya timu hiyo.

Mechi hiyo inatarajiwa kuchezwa Jumapili ijayo, saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Mohamed Hamlaoui.

“Nadhani tutaondoka Jumatano kwenda nchini Algeria kwa ajili ya mchezo huo, hatuna taarifa yoyote kwamba eti kuna timu nyingine inabidi tuondoke nayo,” kilisema chanzo toka ndani ya klabu ya Simba.

Haya yanakuja kutokana na tetesi na baadhi ya wachambuzi na wadau wa soka kupendekeza kuwa timu hizo zingepewa ndege moja ili kwenda kucheza mechi zao na kusubiriana kwani zote zinakwenda kucheza nchini Algeria.

Wakati huo huo, Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, amesema mafanikio yaliyoanza kujitokeza kwenye klabu hiyo yanatokana na uimara wa viongozi wao, wakiongozwa na Mwenyekiti, Murtaza Mangungu.

INAENDELEA UK. 23

## Azam FC yapania kileleni leo

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Azam FC leo kinatarajiwa kushuka kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma kucheza dhidi ya wenyeji wao Dodoma Jiji, katika mchezo wa raundi ya 13 ya Ligi Kuu Tanzania Bara, ambapo kama ikifanikiwa kushinda itaiengua Simba kileleni.

Azam iliyoshinda michezo sita mfululizo hadi sasa, imepania kuendeleza ubabe huo kwa kuifunga Dodoma Jiji na kukaa kileleni mwa msimamo na kuiacha Simba ambayo kwa sasa inaongoza ikiwa na pointi 28.

Ikiwa na pointi 27, iwapo itashinda itafikisha pointi 30, na kushinda mechi saba mfululizo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Rachid Taoussi, amesema ni mara ya kwanza kufika jijini Dodoma tangu aanze kuifundisha timu hiyo, lakini amekiandaa kikosi chake kwa ajili ya kuendeleza mlolongo wa ushindi kwenye michezo yake ya Ligi Kuu.

“Najua mechi haitokuwa rahisi, Dodoma Jiji ni timu ngumu na wanapambana, lakini nasi tunataka kuendeleza ushindi wetu, tuna morali na tuna wachezaji wazuri zaidi,” alisema kocha huyo raia wa Morocco.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Azam FC, Thabit Zacharia, amesema wamefurahi kufika tena Dodoma, jiji ambalo wana historia nalo, kwani ndipo timu yao ilipopandia daraja na kuingia Ligi Kuu.

“Kikosi chetu kiko kamili, wachezaji wetu wote wapo fiti kwa ajili ya mchezo huu. Tumefurahi sana kuwa Dodoma kwa sababu ni sehemu muhimu sana kwetu, ni sehemu ambayo tulipandia daraja mwaka 2007, tukaanza kucheza Ligi Kuu msimu wa 2008/09 na mara zote tukija hapa tunakuwa kwenye wakati

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >